epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumatano Novemba 13, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581859

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

UCHAGUZI MITAA

## Samia aingilia kati wagombea kukatwa



• **Aelekeza** wenye makosa madogo kurejeshwa, Mchengerwa aahidi kufunguka zaidi.. *Endelea Ukurasa 2*

KUCHOMA MKE KWA MAGUNIA YA MKAA

## Korti yapokea udongo wenye masalia mafuta

UKURASA 7



Mshtakiwa wa kesi ya mauaji ya mkewe kisha kumchoma moto kwa magunia ya mkaa, Hamisi Luoga akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, akiingia katika Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dar es Salaam jana, kusikiliza ushahidi wa kesi inayomkabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**



## Kasi wanawake kutumia bangi skanka yashtua

UKURASA WA 3




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

UKURASA WA 5

**Lissu:** Hoja tatu zifanyiwe kazi na CHADEMA katika Uchaguzi S/Mitaa

UKURASA WA 3

**Kundi** 'Walonjoo' tishio, ladhuru watu kwa mapanga na udhalilishaji

UKURASA WA 5

**Uingereza** yatoa bil. 34/- kuboresha huduma za afya

**MICHEZO** **MSUVA ATUA KAMBINI STARS, AONGEZA MZUKA** UK.23

**KATUNI** UK.6



Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, mjini Singida jana, kuhusu masuala ya uchaguzi wa serikali za mitaa. Kushoto ni Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Singida Mjini, Swahiba Mohamed na kulia ni Askofu Mwanamapinduzi, Maxmiliamu Kadutu. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Samia aingilia kati wagombea kukatwa

**Na Gwamaka Alipipi**

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, ameingilia kati malalamiko ya vyama vya upinzani kudai wagombea wao wameenguliwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu.

Rais Samia ameielekeza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kupuuza kasoro ndogo ndogo zilizofanywa na wagombea wa vyama vya siasa wakati wa kujaza fomu kwa ajili ya uchaguzi huo unaohusu serikali za mitaa, vijiji na vitongoji.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uwapo wa wagombea wengi wa vyama vya siasa kuenguliwa kutokana na makosa madogo waliyoyafanya wakati wa kujaza fomu.

"Nilikuwa na kikao na Mwenyekiti wa Chama, Dk. Samia Suluhu Hassan, ambaye ameiagiza TAMISEMI kuyapuuza makosa madogo madogo yaliyojitokeza wakati wa kujaza fomu. CCM inaamini katika demokrasia, hivyo ni wakati wa kuwapa nafasi wale waliokosea kujaza fomu kwa makosa madogo madogo," alisema.

Dk. Nchimbi alisema kuna makosa makubwa ambayo hayakwepeki ambayo TAMISEMI inapaswa kuzingatia sheria, akitolea mfano mgombea kujaza fomu au kushiriki katika kundi la jinsia nyingine.

**Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uwapo wa wagombea wengi wa vyama vya siasa kuenguliwa kutokana na makosa madogo waliyoyafanya wakati wa kujaza fomu.**

Alisema lengo la Dk. Samia ni watu wapate nafasi zaidi ya kujifunza kwamba demokrasia ya nchi bado changa pamoja na kila Mtanzania (mgombea) apate nafasi ya kulitumikia taifa.

"Tunaziomba mamlaka zinazohusika hasa TAMISEMI katika hatua ya mwisho ya rufaa (rufani) kuyapuuza makosa madogo ili Watanzania wengi wapate mafasi ya kugombea," alisema.

Dk. Nchimbi alisema lengo la CCM ni kuona wagombea wengi wa vyama vya siasa wanashiriki kama ilivyokuwa wakati wa kujiandikisha kwa wananchi ili dhana ya demokrasia ya kweli ionekane.

Alisema ni sera ya CCM kuona nchi inastawi kidemokrasia, kunakuwa na utaifa na siasa zenye afya kwa maendeleo ya taifa.

Nchimbi alisema idadi ya mitaa nchini ni 4,265 lakini wapinzani wamesimamisha wagombea 3,256 na CCM wagombea 1,009.

Alisema idadi ya vijiji nchini ni 12,274 vyama vya upinzani vimesimamisha wagombea 5,889, vitongoji ni 63,863 vyama vya upinzani vimesimamisha wagombea 20,000 na CCM wagombea 42,000.

Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

# Waziri: Kuna propaganda katika hoja za upinzani Uchaguzi S/Mitaa

**Na Waandishi wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, amekosoa vikali madai ya baadhi ya vyama vya upinzani kutotendwa haki katika mchakato wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, akidai kuwa hoja zao nyingi zimejawa propaganda zenye lengo la kupotosha umma.

Amesema kuwa kesho ataweka hadharani ushahidi wote kuhusu malalamiko yanayotolewa na vyama hivyo, akisisitiza kuwa vingi vimeshindwa kuwasimamisha wagombea katika maeneo mengi nchini.

Waziri huyo amesema vyama vyote vya siasa vilishirikishwa katika hatua zote tangu kuanza kutengeneza kanuni na utekelezaji wake, na kwamba kila kinachofanyika ni kwa mujibu wa nyaraka hizo, huku wagombea wakitakiwa kutumia vyema muda wa kukata rufani.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waharir wa vyombo mbalimbali nchini kuhusu hatua zinazoendelea kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Kuhusu kufungwa kwa ofisi, alisema hoja ya kwamba ofisi za watendaji zimefungwa kwa lengo la kuwanyima haki wagombea wa upinzani, ni propaganda kwa kuwa zilikuwa wazi muda wote na wagombea walipaswa kurejesha fomu za maombi na kuwasilisha rufani zao kwa kamati husika kwa mujibu wa kanuni.

Mchengerwa alisema kanuni zinatoa rukhsa ya kukataa rufani lakini kinachoendelea hivi sasa ni viongozi wa vyama kitaifa kulalamika, huku wagombea wao wakiwa nyumbani, hawakati rufani kama kanuni zinavyoelekeza.

Alisema baadhi ya vyama vinatumia muda mwingi kufanya propaganda kwa kusambaza taarifa kwenye mitandao ya kijamii badala ya kufuata utaratibu wa kikanuni ambao umewekwa.

"Nilisikia eti Iringa na Kilimanjaro wagombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wameondolewa, hii si kweli! Novemba 14, 2024 nitatoa taarifa za kina na ushahidi wote kuhusu mchakato huu.

"Vyama havikujiandaa na kupelekea kutoa nafasi kwa chama kimoja kugombea. Mfano, katika wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, kuna vijiji 60, CCM ilisimamisha wagombea wote ila CHADEMA ilisimamisha wagombea 30 pekee. Sasa hawawezi kulingana na CCM katika kupata wagombea.

"Hatua tuliyonayo ni ya propaganda ya siasa, waandishi mjitenge na propaganda hizi. Mfano, diwani mstaafu aliandika kule Rufiji waliweka wagombea katika vijiji 32 na wote wakakatwa, jambo ambalo ni uongo, halmashauri hii ina vijiji 38 na CHADEMA ilisimamisha wagombea wawili," alisema.

Waziri Mchengerwa alisema Dar es Salaam ina mitaa 564, lakini diwani huyo mstaafu (akimlenga Boniface Jacob) amesema kuna mitaa 600, lakini CHADEMA hawakusimamisha wagombea katika mitaa yote huku wakieneza taarifa alizoziita "za uongo".

Kuhusu tafsiri ya umri, waziri huyo alisema kuna walioandika wamezaliwa mwaka 2024, ikiwa na maana hawaruhusiwi kugombea, na kwamba katika hilo, wamo pia wagombea wa CCM walioondolewa kwa kigezo cha kukosea tarehe na mwaka wa kuzaliwa.

"Mfano, Manispaa ya Kigoma Ujiji wagombea wa ACT Wazalendo walioenguliwa ni 11 na 58 walipitishwa, ila taarifa zao ni kwamba wagombea wote wameondolewa. 11 walifuata taratibu za kanuni wakakata rufani na watano walirejeshwa, na sita waliondolewa kwa changamoto ya umri, ukazi, kutojiandikisha na udhamini," alisema.

Mchengerwa ambaye ni Mbunge wa Rufiji, alisema kuwa hata CCM kuna mgombea wao alijaza amezaliwa Oktoba 2024 na kwamba alienguliwa na hakuna upendeleo, bali utekelezaji kanuni.

"'Kuposti' kwenye mitandao hakutakisaidia chama, Katiba imeweka mifumo mizuri ya kutenda haki, wafuate taratibu," alisema Waziri Mchengerwa.

Alisema wanasiasa waelezwe ukweli na kuachana na propaganda ambazo zitaligawa taifa, na kwamba si kweli kwamba vyama vimeondolewa kwa kuwa yapo maeneo hawajasimamisha wagombea na wanadanganya umma kwamba wamesimamisha wagombea waKaenguliwa.

"Hatuwezi kuwa na taifa tunatunga sheria, tunazibadili wenyewe bila kufuata utaratibu. Vyama vyote vilishirikishwa katika kutunga kanuni hizi zinazofanya kazi.

"Waambieni wanasiasa wafuate misingi ya kanuni, sheria na Katiba, tutakuwa na taifa la ovyo ikiwa tutawaaminisha wanasiasa kuwa wanaweza kwenda kinyume," alisema.

Awali, Ofisa wa Sheria wa TAMISEMI, Mihayo Andrew alisema moja ya masharti ya wagombea katika kanuni za uchaguzi huo ni kuwa na shughuli halali inayomwezesha mgombea husika kuingiza kipato.

Alisema hakuna tafsiri ya shughuli halali, lakini kwa akili ya kawaida ni yoyote ambayo inafanyika kwa mazingira halali na kumpa mtu kipato halali.

"Anapata kipato cha kukidhi mahitaji yake, zinatambulika na mamlaka kisheria na kwamba ujasiriamali ni shughuli inayotambulika kisheria," alisema.

Alisema kuwa yeyote ambaye alijaza ujasiriamali na jina lake likakatwa anapaswa kukata rufani kwa kamati husika.

"Tangu kubandikwa kwa wateule, vyama vya upinzani vimelalamikia wagombea wao kukatwa bila sababu za kueleweka, na wachache waliobakia waliwekewa mapingamizi na wagombea wa vyama vingine walioshinda," alisema.

Alisema sifa za mgombea ni awe mkazi kwenye kijiji au mtaa wake, awe Raia wa Tanzania, awe na umri wa miaka 21, ajue kusoma, kuandika lugha ya Kiingereza na Kiswahili, na adhaminiwe na chama chake cha siasa.

Ofisa huyo pia alisema ikiwa mgombea hakujiandikisha katika Daftari la Wakazi, anapoteza sifa za kugombea kwa kuwa anapaswa kuwa mfano kwa wengine.

HABARI KITAIFA

# Kasi wanawake kutumia bangi skanka yashtua

**Na Zanura Mollel**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imebaini kuna ongezeko la wanawake wengi kununua na kutumia dawa za kulevya aina ya skanka ambayo ni aina ya bangi.

Wamesema kundi hilo hutumia dawa hizo kwa sababu mbalimbali zikiwamo migogoro ya kimapenzi, msongo wa mawazo na wengine kuzitumia kwa starehe.

Kamishna Jenerali wa Malamka hiyo, Aretas Lyimo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akiwasilisha taarifa ya operesheni iliyofanyika nchi nzima kati ya mwezi Oktoba na Novemba, mwaka huu.

Lyimo alisema skanka ni aina ya bangi yenye kiwango kikubwa cha sumu na husababisha madhara zaidi kiafya.

"Wauzaji waliokamatwa walipohojiwa soko lao kubwa, walieleza kuwa wanunuzi wengi ni wanawake hata hivyo utafiti uliofanyika kwa baadhi ya saluni na kundi la wadada watumiaji, walidai kuwa skanka inawapunguzia mawazo na wakati mwingine huwasababishia uraibu.

"Hutumia kwa sababu ya msongo wa mawazo kutokana na hali ngumu ya maisha pamoja na usaliti katika mapenzi.

"Kwa wanawake walioshindwa kumudu hali hiyo wamejikuta wakitumia dawa hiyo kama suluhisho na hii ni baada ya heroin kupungua kwa kiasi kikubwa nchini kutokana na matokeo ya udhibiti," alisema.

Kamishna Lyimo alisema heroin kwa sasa imepungua na inayopatikana imebainika kuchanganywa na vitu vingine kama unga wa dona pamoja na masega, hivyo hupoteza uwezo kwa watumiaji na kuwalazimu wengi wao kuingia katika matumizi ya skanka.

"Pamoja na udhibiti huo lakini bado watumiaji wameanza kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya ambazo hutumika kwa wagonjwa wa saratani na wale wenye maumivu makali kama mbadala wa dawa za kulevya.

"Hata hivyo, serikali inaweka utaratibu maalum wa kudhibiti dawa hizo kutouzwa katika kila duka la dawa lengo ni kupunguza ongezeko la waraibu.

Kamishna Lyimo alisema katika operesheni hizo walikamata kilogramu 1,066.105 za dawa za kulevya, mililita 447 za dawa tiba zenye asili ya kulevya na kuteketeza jumla ya ekari 157,4 za mashamba ya bangi na lita 19,804 za kemikali bashirifu pamoja na kuwakamata watuhumiwa 58.

Alisema kati ya dawa hizo, kilogramu 687.32 za skanka na kilogramu moja ya hashishi zilikamatwa eneo la Goba, Dar es Salaam, zikiwa zimefichwa ndani ya nyumba ya mtuhumiwa.

Alisema hashishi hutengenezwa kwa mchanganyiko wa maua na mafuta ya mbegu za bangi na inapovutwa huzalisha kemikali hatari zinazosababisha magonjwa ya akili kwa haraka.

"Katika uwanja wa ndege wa Mwalimu Julius Nyerere mamlaka imekamata mililita 120 za dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Codein zikiwa zinasafirishwa kwenda nje ya nchi pamoja na mililita 327 zilizokutwa nyumbani kwa mtuhumiwa eneo la Tabata Kinyerezi, Dar es Salaam.

"Dawa hizo ziliingizwa nchini kinyume na taratibu zikiwa zimeweka chapa bandia ya dawa za kuogeshea mbwa na paka ili kuepuka kubainika," alisema Kamishna Lyimo.

Alisema jijini Dodoma wamekamatwa watuhumiwa wawili, Suleiman Mbaruku (52) maarufu Nyandana na Kimwaga Lazaro (37) wote wakazi wa Mtaa wa Kinyali, Kata ya Viwandani, ambao wamekamatwa na jumla ya gramu 393 za heroin.

"Nyanda, ni kinara wa biashara ya dawa za kulevya mkoani humo na alikuwa akifuatiliwa kwa muda mrefu, hata hivyo waraibu wengi walioko katika Kituo cha Itega kinachohudumia watu wenye uraibu, yeye ndiye kawaharibu na dawa hizo," alisema Kamisha Lyimo.

Alisema kupitia operesheni za kanda wamekamata kilo 303.553 za bangi, gramu 103.8 za heroin na kilo 63 za mirungi katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema mamlaka imebaini baadhi ya wafanyabiashara wa shisha huchanganya dawa za kulevya pasipo wateja kufahamu lengo likiwa ni kuimarisha biashara zao.

"Utafiti na sampuli zilizochukuliwa umeonesha baadhi ya wafanyabiashara kukiuka sheria za nchi. Tunatarajia kuiweka shisha katika udhibiti," alisema Kamishna Lyimo.

Katika hatua nyingine, Kamishna huyo alitaja changamoto zinazowakabili katika utendaji kazi ni uwapo wa vipenyo vingi katika mipaka ya nchi hivyo watu wasiowaadilifu hutumia kama njia ya kuvusha dawa za kulevya.

"Rushwa na mfanyabiashara wa dawa za kulevya ni kitu kimoja. Tumeingia makubaliano na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (TAKUKURU) ili tuweze kushirikiana kudhibiti hali hii.

"Unakuta shamba la bangi au mirungi katika eneo ambalo kuna viongozi wa serikali, unajiuliza hawakuliona hili? Lakini pia katika mipaka inavukaje kwa magari ya mizigo wakati wapo watu wa ukaguzi," alisema.

# Kundi 'Walonjoo' tishio, ladhuru watu kwa mapanga, udhalilishaji

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA Kijiji cha Churuku, Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma kumeibuka kikundi cha vijana wanaojiita 'Walonjoo' wanaodaiwa kufanya matukio ya uhalifu wa kujeruhi wananchi kwa mapanga na kuwadhalilisha.

Kikundi hicho ambacho kinadaiwa kutumika kuchunga na kulinda mifugo porini kimekuwa kikifanya matukio hayo mara kwa mara hasa kupigana wao kwa wao na kujeruhiana.

Hivi karibuni Nipashe ilipata taarifa ya kuwapo kwa tukio la mauaji ya mtu mmoja na wengine watatu kujeruhiwa na kundi hilo na kusababisha wananchi wa eneo hilo kuhofia usalama wao.

Mmoja wa wananchi ambaye jina lake limehifadhiwa, alisema kundi hilo limekuwa ni kero kwa wananchi wa kijiji hicho hali inayosababisha waishi maisha ya hofu.

"Maisha ya vijana hawa ni porini na hulala katika mazizi ya ng'ombe, ukiwaona wamejifunga mashuka ya kimasai, lakini sio wamasai ni vijana wakirangi, matukio wanayofanya yamekuwa tishio, wakiwa na vurugu za kutofautiana huko wanakuja kijijini kama kulipiza kisasa," alisema.

**MAJERUHI WAFUNGUKA**

Mmoja wa majeruhi aliyelazwa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma, Athuman Makha, anayeishi Kiteto, anasimulia yaliyompata baada ya kwenda jijini huko kusalimia wazazi wake.

Alisema wakati akitoka matembezini usiku alikutana na na kikundi cha vijana takribani 30 ambao walikuwa na mapanga na kuanza kumshambulia, kitendo ambacho hadi leo hajui tatizo ni nini.

"Wamenishambulia wamenivunja mkono na mguu kama unavyoona umetolewa, hapa shavuni na mikwaruzo maeneo mengine ya mwili.

"Hadi sasa sijasikia kama kuna watu wamekamatwa. Mbona imekuwa kimya, ninaomba serikali ichukue hatua," alisema.

Alisema vijana hao ambao wanajiita Maronjoo bado wapo kijijini na haoni taarifa yoyote.

Akizungumza kwa tabu kutokana na maumivu aliyonayo, Shariff Makha, anasimulia namna alivyokumbwa na mkasa huo usiku wakati akiwa amelala baada ya kusikia watu wanabomoa nyumba yake.

"Walianza kubomoa nyumba yangu, nikajiuliza kuna nini? Mbona hawa watu wanaharibu? Nilisikia sauti ikisema, 'bomoeni haraka haraka ili tumkute tumpige'.

"Walipoingia waanza kunishambulia kwa panga, nilipiga kelele wakati wakiendelea kunishambulia maeneo mbalimbali ya mwili, nikaishiwa sauti na kupoteza fahamu nikiwa hapo kitandani."

"Sikujua kumbe nje kulikuwa na watu wamekuja kuniokoa, walishuhudia watu wakitoka wakikimbia, ndipo wakanichukua na kunikimbiza hospitalini, nimepata fahamu nikiwa hospitalini," anasimulia mkasa wake," alisema.

Abdi Saidi, alisema akiwa amelala usiku alisikia kelele kwa jirani yake na alipotoka nje ili kujua kuna tatizo gani, alikuta watu wengi wakimshambulia jirani yake na alipowahoji, mmoja wa vijana hao alimkimbilia na kumkata na panga mgongoni.

"Vijana hawa walisikika kufanya matukio ya kuvamia watu na kujeruhi, ni vijana wa kijijini humo, hawa vijana wanajulikana kama 'walonjoo' wanajifunika mashuka kama masai na ni watoto wa kirangi wanaofanya hivi," alisema.

Mtendaji wa Kijiji hicho, Issa Nterukwa na Diwani wa Kata ya Churuku, Daudi Manyika, wamekiri kuwapo na matukio yanayofanywa na kundi hilo, lakini hawakuwa tayari kuzungumza kwa kina na kutaka mwandishi wa habari awatafute wenye mamlaka ya kuzungumza.

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, George Katabazi, akizungumzia matukio hayo, alisema vijana hao ni wahalifu wa kawaida wanaojishughulisha na uchungaji mifugo porini na wakati mwingine hufanya vurugu za kugombana wao kwa wao.

"Katika tukio hili walifanya vurugu za kugombana wao kwa wao kule pori na walipogombana walikuwa wanalipiza kisasi katika lile kundi jingine la vijana na huyo mtu aliyeuawa alikuwa anaamua ugomvi wa hao vijana," alisema.

Alisema tayari Jeshi la Polisi linawashikilia watu watatu na watafikishwa mahakamani.

"Hili group (kundi) ambalo wanalitumia kulinda au wakati wa kuchunga mifugo huko porini, kwa hiyo kwa kuwa wakati mwingine wale ni vijana huwa wanafanya vurugu kugombana wao kwa wao na wanaanza kuwindana kama vijana, kwa hiyo ndugu wakiingilia ndio wanajichukulia sheria mkononi," alisema.

Kamanda Katabazi alisema tayari wamewaambia wananchi atakayefanyiwa vurugu na hao vijana watoe taarifa Kituo cha Polisi.

"Maana ukute watu wanasema hao wanatuumiza wanatufanya nini, wanatushambulia, lakini wakiambiwa mmetoa taarifa polisi unakuta matukio hayo hawatoi taarifa polisi.

"Kama wakitoa taarifa polisi sisi tutachukua hatua, kama hao waliofanya vurugu watuhumiwa watatu tayari tumewakamata tunaendelea kuwahoji na wengine tunaendelea kuwatafuta," alisema.

Aliwataka wananchi pindi wanapofanyiwa vurugu na kundi hilo watoe taarifa kwa wakati polisi wachukue hatua na si kufumbia macho vurugu hizo.

"Sisi tutakapopata taarifa tutakuwa tunachukua hatua, kikubwa wananchi wasikae kimya wanapoona mambo kama hayo, wafike polisi sisi tutachukua hatua stahiki," alisema.

Kwa maoni kuhusu habari hii: Sms / WhatsApp : +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu (kushoto), akibadilishana taarifa za makubaliano na Mkurugenzi wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini, Kemi Williams, baada ya Uingereza kuipatia wizara hiyo paundi milioni 10 sawa na Sh. bilioni 34.28, kwa ajili ya Mfuko wa Afya (Health Basket Fund-HBF), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Rais Samia: Mafanikio ya wanafunzi faraja kwa wazazi

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mafanikio ya wanafunzi wanaofanya mitihani, yatakuwa faraja kwa walimu, wazazi na Watanzania wote.

Amesema kupitia ulipaji kodi na utunzaji wa amani na utulivu wa nchi, wanaiwezesha serikali kuendelea kutekeleza mipango inayojiwekea, ikiwamo kutoa elimu bila malipo.

Rais Samia aliyasema hayo kupitia taarifa aliyoichapisha kwenye ukurasa wake wa X, akisema mafanikio hayo yataiwezesha pia serikali kukamilisha kazi mpya aliyoianza ya kuboresha mfumo wa elimu ili kuendana na mazingira na mahitaji ya sasa.

Aidha, Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Dk. Said Mohamed, alisema wakati Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne (CSEE) ulioanza juzi, wanafunzi 161,020 sawa na asilimia 23.3 waliopaswa kuufanya hawatakuwa wahitimu.

"Kila la kheri wanafunzi wote wa kidato cha nne mnapoanza mtihani wa kuhitimu (CSEE). Nawaombea utulivu na mafaniko katika hatua hii muhimu ya kujiandaa kushiriki vyema kwenye nguvu kazi ya familia, jamii na Taifa kwa ujumla," alisema Rais Samia.

Mmoja wa wazazi ambao watoto wao ni watahiniwa Ezekiel Magoto, alisema: "Mzazi yeyote anapambana na kuhakikisha anatimiza wajibu wake wa kumpatia mwanawe elimu ikiwamo kumlipia ada, mara zote matarajio yake makubwa ni kuona mtoto anafanya vizuri na si vinginevyo."

Pia alisisitiza wanafunzi wanaoshiriki katika mtihani huo kuhakikisha wanafuata sheria na kanuni zote zinazowaongoza na kujiepusha na udanyanyifu ambao unaweza kusababisha kushindwa kukidhi vigezo na hatimaye kuharibu mustakabali wao kielimu.

Dk. Mohamed alisema mwaka juzi wakati wanafunzi hao wanafanya Mtihani wa Kidato cha Pili walikuwa 690,341 lakini walioandikishwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne 2024 ni 529,321.

"Kuna upungufu wa takribani wanafunzi 161,000 waliofanya mtihani kidato cha pili ambao walitakiwa kufanya mtihani huu wa kidato cha nne na hawapo katika orodha ya waliosajiliwa mwaka huu," alisema.

Akizungumzia mtihani wa kidato cha nne mwaka huu, Katibu Mtendaji huyo alisema watahiniwa 557,731 wamesajiliwa kufanya. Kati yao, watahiniwa wa shule ni 529,321 na wa kujitegemea ni 28,410.

Pia alisema kati ya watahiniwa wa shule waliosajiliwa mwaka huu, wavulana ni 250,562 sawa na asilimia 47.34 na wasichana ni 278,759 sawa na asilimia 52.66.

**ABBOTT FUND TANZANIA**

(NGO Certificate of Registration Number 00483)

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON-GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT (AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations requires that all non-governmental organisations in Tanzania publish biannually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE**, we wish to make the following public disclosure of the funds approved for 2024 activities and their proposed expenditure, which publication covers the reporting period from **1st July 2024 to 31st December 2024:**

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Leadership Capacity-Building. | 110,000.00 |
| **Emergency Medicine Regional and District Amplification:** Includes support to MNH Emergency Medicine, and EMD infrastructure project. | 600,000.00 |
| **Village Emergency Care Model** in Dodoma, Mbeya and Tanga. | 375,000.00 |
| **Building Livelihoods**: Includes support to National Children's Centre in Dodoma. | 285,000.00 |
| **Mapatano Project:** Includes infrastructure project at Mapatano Secondary School. | 2,246,000.00 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff. | 1,986,000.00 |
| **Total Funds received from Abbott Fund, Chicago IL, USA for the year 2024.** | **5,602,000.00** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA**

# Mvutano waibuka kortini kisa kielelezo cha bangi

**Na Kulwa Mzee**

MVUTANO umeibuka Mahakama Kuu Divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi baada ya mawakili wa utetezi kupinga kilo 126.36 za bangi kupokewa kama kielelezo.

Hatua hiyo ilitokea baada ya upande wa Jamhuri kuomba mahakama ipokee kwa kuwa anayeomba kutoka ana uwezo wa kufanya, hivyo mapingazi yatupwe hayana mashiko.

Mawakili wa utetezi walidai kilo hizo za bangi hazikusomwa wakati wa ushahidi katika Mahakama ya Temeke, hivyo shahidi hana uwezo wa kutoa kielelezo hicho mahakamani na alikosea kuelezea kielelezo kabla hakijapokelewa na kuomba kisipokewe.

Hayo yaliibuka jana mahakamani hapo mbele ya Jaji Godfrey Isaya wakati shahidi wa kwanza katika kesi ya kusafirisha dawa za kulevya inayomkabili Juma Bakari, akitoa ushahidi na kuomba kielelezo kipokewe kama sehemu ya ushahidi wake.

Shahidi kutoka Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Theodory Ludanha, aliongozwa kutoa ushahidi wake na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Erick Shija.

Upande wa utetezi uliwakilishwa na mawakili Nehemiah Nkoko na Jeremiah Mtobesya .

Akiwasilisha pingamizi, Wakili Nkoko alidai wana hoja tatu za kupinga kielelezo hicho kupokewa mahakamani.

Nkoko alidai kuwa wakati wa kusomwa maelezo ya mashahidi katika Mahakama ya Temeke, kielelezo hakikusomwa, hivyo inamnyima nafasi mshtakiwa kujitetea.

Wakili Nkoko alidai kuwa shahidi ametoa mahakamani mifuko 10 yenye pakiti 144 zenye jumla ya kilo 126.36 za bangi wakati hayo maelezo hayakutolewa katika mahakama ya chini.

"Ni takwa la kisheria kusoma maelezo hayo wakati wa kusoma ushahidi ili kumsaidia mshtakiwa kuandaa utetezi. "Mheshimiwa Jaji hakuna notisi yoyote iliyotolewa kutaja vielelezo ambavyo havikuelezewa katika maelezo ya mashahidi, hivyo tunaomba visipokewe," alidai Nkoko.

Akiwasilisha hoja nyingine, Wakili Mtobesya alidai katika sheria inaeleza nani anatakiwa kutoa kielelezo mahakamani na kwamba anayestahili ni polisi aliyekutana mara ya kwanza na kielelezo au mtu mwingine aliyekuwa na mamlaka ya kipolisi.

Alidai kuwa shahidi hana uwezo wa kutoa dawa hizo kama kielelezo mahakamani kwa sababu anaeleza katika ushahidi wake alipokea kutoka kwa Zuwena Hatibu.

Wakili Mtobesya alidai kuwa shahidi wakati wa ushahidi wake alikwenda mbali zaidi ya alichotakiwa kufanya mahakamani.

"Sheria inaeleza kwamba maelezo ya kitu yataingia kwenye kumbukumbu za mahakama baada ya kupokewa kama kielelezo mahakamani lakini shahidi katika kesi hii katoa maelezo kisha anaomba dawa zipokewe.

"Shahidi alieleza kuhusu majani na kwamba alipofanya uchunguzi alibaini kuwa yalikuwa bangi, maelezo hayo hayakutakiwa kuingia katika kumbukumbu za Mahakama kabla ya kupokelewa kielelezo," alidai Mtobesya.

Wakili Mtobesya aliomba mahakama ikubali hoja zao tatu za pingamizi kuzuia kielelezo kupokewa kabisa na kwamba shahidi anayeomba kutoa hana uwezo wa kuomba kufanya hivyo.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Shija, alidai kuwa kielelezo kinachoombwa kutolewa kilielezwa wakati wa kusomwa maelezo ya mashahidi na utaratibu ulifuatwa na kwamba Mahakama ya Rufani ilielekeza kuwa yeyote ambaye kielelezo kilipitia mikononi mwake anaweza kutoa ushahidi.

"Shahidi ana sifa ya kutoa kielelezo hicho mahakamani kwa sababu alichunguza , alifunga kwenye lakiri na kumrudishia Zuwena Hatibu.

"Shahidi wakati anatoa ushahidi alikuwa anatengeneza msingi wa namna anavyoweza kutambua kielelezo na kipindi chote cha ushahidi alieleza atatambua kielelezo kwa lakiri ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kwa saini yake, tarehe ya uchunguzi, muhuli wa maabara na alieleza rangi ya vifungashio na si kwamba akizungumzia ushahidi,"alidai Wakili Shija.

Anadai shahidi alieleza picha ya kutambua na baada ya kutambua pakiti zote ndipo alipoomba vipokelewe kama ushahidi wake mahakamani, hivyo kuomba hoja za pingamizi kutupiliwa mbali.

Baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, mahakama iliamuru kutoa uamuzi wa kupokea ama kukataa kupokea kielelezo hicho leo.

## Uingereza yatoa bilioni 34/- kuboresha huduma za afya

**Na Christina Mwakangale**

UINGEREZA imetoa paundi milioni 10 sawa na Sh. bilioni 34.28 kwa ajili ya Mfuko wa Afya (Health Basket Fund-HBF), ili kuboresha huduma za afya kuanzia ngazi ya msingi.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, aliwekeana saini na nchi hiyo jana jijini Dar es Salaam huku nchi hiyo ikiwakilishwa na Mkurugenzi wa Maendeleo kutoka Ubalozi wa Uingereza nchini, Kemi Williams.

Mfuko huo maalumu ulianza mwaka 1999, umekuwa ukikusanya fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo, kwenda kuboresha huduma za afya nchi nzima kuanzia ngazi ya huduma za msingi, zikiwamo zahanati.

Akizungumza baada ya kuingia makubaliano hayo, Dk. Jingu alisema fedha hizo zitatumika kwa kipindi cha miaka mitano 2024 - 2029 kwenda kuchangia huduma bora za afya.

"Waanzilishi wa mfuko huo mwaka 1999 walikuwa serikali za Uingereza, Denmark, Uswizi, Norway na Ireland pamoja na Benki ya Dunia (WB) lakini baadaye Uingereza ilijitoa. Mwaka 2021 tukaanzisha mpango wa miaka mitano kukubaliana na wadau mbalimbali na wakaongezeka wengine.

"Wakafikia tisa pamoja na hawa wa awali, wakaingia UNICEF, KOICA na Canada. Uingereza sasa mwaka huu wamerudi wakisema jambo walilolianzisha mwaka 1999 wanaendelea nalo. Kwa miaka 10 paundi milioni 10 kila mwaka watatoa paundi milioni mbili, tunafurahia kuendelea nao katika safari hii," alisema Dk. Jingu.

Alisema mfuko huo ambao tayari una wadau waliochangia fedha hizo zilizotolewa na Uingereza jana, zinakuwa nyongeza kwa HBF na kwenda kuimarisha huduma za afya na kuunga mkono huduma ya bima ya Afya kwa Wote.

"Tunaimarisha upande wa mahitaji ili huduma ziwe imara na bora, upatikanaji wake, zipatikane nchi nzima zikiwa na ubora," alisema Dk. Jingu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, alisema wizara hiyo itahakikisha inatoa fedha hizo kwa wakati kwa Wizara ya Afya ili kufanikisha utekelezaji wa mradi.

"Mradi huu ni kuanzia mwaka 2024 hadi 2029. Tutahakikisha fedha hizi zinatumika kwa malengo yaliyowekwa na si vinginevyo," alisema Dk. Mwamba.

Mkurugenzi wa Maendeleo wa Ubalozi wa Uingereza nchini, Kemi Williams, alisema kurejea kwenye mradi huo ni furaha na si kwa lengo la kutoa fedha kwenye mfuko huo tu, bali ni kurejea upya kwenye ushirikiano.

"Tutahakikisha tunashirikiana na Tanzania kufikia azma ya Tanzania ya huduma ya bima ya Afya Kwa Wote, kila mmoja ana haki ya kupata huduma ya afya," alisema Kemi.

Naye Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Grace Magembe, alisema asilimia 90 ya fedha za HBF zinatumika katika huduma za msingi za afya, ikiwamo tiba nchini kote.

Pia alibainisha kuwa takribani asilimia 80 ya wananchi wanahudumiwa na huduma mbalimbali kutoka kwenye mfuko huo, kupitia zahanati, vituo vya afya na hospitali.

Alisema asilimia 60 hadi 70 ya huduma za afya ya msingi zinazotolewa kwenye maeneo yao zinategemewa na wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka mitano pamoja na vijana.



Mkuu wa Wilaya ya Lushoto, mkoani Tanga, Zephania Sumaye (kulia) na Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Dk. Ikupa Mwaysoge, baada ya kukabidhi vitimwendo vitano kwa watoto watano wenye mahitaji maalum, vilivyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Lissu ameishauri CHADEMA kudai hoja tatu uchaguzi Serikali za Mtaa

**Na Waandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, amekitaka chama chake kujipanga upya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kudai hoja tatu za msingi.

Amedai kutegemea kupata ushindi itakuwa vigumu kutokana na figisu zilizoko ambazo zimesababisha wagombea wengi wa upinzani kuenguliwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mjini Singida, Lissu alitaja hoja za msingi ambazo chama hicho kinapaswa kuzisimamia kwa sasa ili kuleta mafanikio katika chaguzi zijazo ni kudai Katiba Mpya, mfumo huru wa uchaguzi na Tume Huru ya Uchaguzi.

"Kitendo cha kuwaengua wagombea wengi wa upinzani maana yake ni kama uchaguzi umekwisha, hao masalia ya wagombea wa upinzani waliobaki sawa, lakini tunahitaji tujipange upya uchaguzi umevurugwa yaliyotokea uchaguzi wa 2019 yametokea uchaguzi wa mwaka huu," alidai.

Lissu alisema wagombea wengi wa CHADEMA wameenguliwa na sababu za mapingamizi yaliyowekwa, akidai yanafanana nchi nzima.

Alisema pingamizi kwa wagombea wa upinzani ziliwekwa na wasimamizi wa uchaguzi na sio na wagombea, jambo ambalo ni kinyume cha sheria ya uchaguzi.

"Mapingamizi mengi yamewekwa kuanzia Novemba 8, mwaka huu, wakati ilikuwa ndio siku ya kuteua wagombea.

"Maana yake wagombea waliwekewa mapingamizi hata kabla majina yao hayajabandikwa, swali je, walijuaje na sababu za mapingamizi ni zilezile," alidai.

Lissu alisema siku nne zilizowekwa za kujibu mapingamizi kwa nchi nzima ni vigumu kutokana na wagombea wengi wa upinzani kuwekewa mapingamizi, itakuwa ngumu kufikia hata asilimia tano ya kujibu pingamizi kwa wagombea walioenguliwa.

"Watu walioenguliwa ni zaidi ya 100,000, je, wote wataweza kukata rufani na rufani zao zisikilizwe ndani ya siku nne. Mimi mwenyewe (Lissu) sijalala kushughulikia rufani katika kajimbo kamoja tu Singida Mashariki, je, itawezekana kwa nchi nzima.

"Ukiniuliza je, kuna namna yoyote ya kuokoa uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa haipo labda tuanze mchakato upya wa uchaguzi, jambo ambalo ninajua serikali haiwezi kukubali," alisema.

Lissu alisema ndani ya chama chake kama kuna mtu anategemea kupata nusu mkate, kupewa uwaziri kwa kukubali figisu zinazofanyika katika uchaguzi wa serikali za mitaa atakuwa anaota ndoto ya mchana.

"Kwa ushahidi huu wa mambo yaliyojitokeza katika uchaguzi huu, tumejitahidi kurudi nyuma sasa kutaka twende mbele ni kujitakia anguko mbeleni. Cha msingi ni kukazania hoja ya Katiba Mpya, Tume Huru ya Uchaguzi na mfumo huru wa uchaguzi," alisisitiza.

**MARIDHIANO**

Akizungumzia kuhusu maridhiano yaliyofanyika kati ya serikali na vyama vya siasa, Lissu alisema kuna makosa kama chama walifanya kukubaliana na jambo hilo.

"Kuna makosa mengi tuliyafanya ndio maana mimi nilishiriki mikutano miwili tu ya maridhiano nikagundua hapa tunadanganywa," alidai.

**KUTOJIANDIKISHA**

Kuhusu kutojiandikisha kupiga kura kijijini kwake wilayani Ikungi, Lissu alisema hiyo ilitokana na kuwa nje ya nchi kushughulikia suala la kufungua kesi ya kampuni fulani ya simu.

Lissu alisema hata hivyo hata kama angejiandikisha kusingeondoa alichokiita figisu zilizojitokeza dhidi ya wagombea wa upinzani kuondolewa kwa mizengwe.

"Mwaka 2019 nilijiandikisha lakini haikuzia wagombea wa CHADEMA kuenguliwa kwa mizengwe," alisema Lissu na kuongeza kuwa aliyoongea ni ya kwake hayajatokana na kikao chochote cha chama na kwamba atapigania uwe ndio msimamo wa chama.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Wilaya ya Singida Mjini, Swahiba Mohamed, alisema Jimbo la Singida Mjini katika nafasi za kugombea uenyekiti wa mitaa, kati ya mitaa 50 waliyoweka wagombea wameenguliwa na kubaki 18, vitongoji wamebaki 23 na vijiji wamebaki watano tu.

***Imeandaliwa na Thobias Mwanakatwe na Elisante John (SINGIDA)**

Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701
Email: customerrelations@guardian.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Upatikanaji wa mbolea uwe wa uhakika msimu wa kilimo

**MVUA** ya kwanza ni ya kupandia. Huu ni msemo wa miaka mingi ambao unawakumbusha wakulima kujiandaa katika shughuli zao za kila siku na pia kuhakikisha wanautumia msimu kwa umakini ili kupata mazao ya kutosha.

Kama ilivyo ada, hivi sasa mvua imeanza kunyesha katika maeneo mengi nchini na huu ndio msimu wa wakulima katika sehemu hizo kuanza kulima mashamba yao na kupanda mazao ya chakula kama mahindi. Ni msimu ambao ni muhimu katika kuelekea kupata mazao mengi kwa ajili ya chakula na mengine kuuza ili kujikwamua kiuchumi.

Kutokana na ukweli huo, wakulima wanasisitizwa kuanza kutumia mvua inayonyesha kupanda mazao katika mashamba waliyoyaandaa kwa ajili ya kilimo. Kwa wale ambao huchelewa au kuzembea kuandaa mashamba, hujikuta katika mazingira magumu kwa kuwa watapata mavuno kidogo au kuambulia patupu na kukutana na msemo kwamba majuto ni mjukuu.

Ni msimu ambao ni wa muhimu kwa wakulima ndiyo maana hata serikali imekuwa ikisisitiza kwa viongozi wa mikoa na wilaya kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo unakuwa wa kutosha na wa bei iliyowekwa.

Msisitizo huo wa serikali unatokana na ukweli kwamba usalama na upatikanaji wa chakula ni miongoni mwa sababu za kustawi kwa amani na utulivu. Pia serikali imekuwa ikisisitiza hivyo kwa sababu sekta ya kilimo inaajiri Watanzania wengine, hivyo ni chanzo cha kuwawezesha watu wengi kujipatia kipato kwa kuuza mazao yao baada ya kuvuna kisha kijikomboa na umaskini wa hali na wa kipato.

Kutokana na ukweli huo, wakati wakulima, pamoja na wengine walioko katika ajira rasmi ambao hujishghulisha na kilimo biashara, wanahamasika kuhakikisha wanatimiza wajibu wao, ni vyema upatikanaji wa pembejeo kwa maana ya mbolea ya kupandia na kukuzia na viuatilifu ukawa wa kutosha. Wakuu wa wilaya na mikoa wanapaswa kuhakikisha kuwasimamia maofisa kilimo na wakurugenzi wa halmashauri ugawaji wa pembejeo hasa mbolea ufanyike bila kasoro yoyote.

Kama wahenga wasemavyo katika msafara wa mamba kenge wamo, wakati msimu wa kilimo unapowadia, kuna wajanja hujitokeza na kuingilia mchakato wa mauzo ya mbolea kwa bei ya juu tofauti na ile iliyopangwa na serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA). Watu hao hununua mbolea kwa bei elekezi kisha kuilangua kwa bei ya juu kwa wakulima, hivyo kuwafanya wapate uchungu wa kuingia gharama kubwa.

Watu hao ambao baadhi yao hijivika kofia ya mawakala, hishirikiana na baadhi ya maofisa wa serikali hasa watendaji wa idara ya kilimo katika halmashauri kulangua mbolea na kuificha na baadaye kuiuza kwa bei kubwa au ya magendo.

Kwa mantiki hiyo, ni wakati sasa wa wakuu wa mikoa na wilaya kuamka na kuanza kusimamia kikamilifu upatikanaji wa mbolea ili wakulima wasihangaike kuipata au kuuziwa kwa bei ya magendo tofauti na ile iliyowekwa. Aidha, kusimamia ugawaji pekee hakutoshi bali kinachotakiwa pia ni kuwatambua mawakala katika maeneo husika na kuhakikisha wanauza kwa kufuata taratibu.

Katika misimu kadhaa iliyopita, suala la kukosekana kwa mbolea au upungufu tofauti na kiasi kinachotakiwa lilijitokeza sana kwenye baadhi ya maeneo, hivyo kusababisha wakulima kukosa pembejeo hizo na kupata mazao kwa kiwango kidogo. Hali hiyo ilisababisha wale wenye uwezo kumudu kununua mbolea kwa gharama kubwa na wale wasio na uwezo kushindwa kumudu.

Suala la mbolea ni nyeti sana katika msimu huu wa kilimo, hivyo serikali kupitia taasisi zake zinazosimamia upatikanaji na usambazaji wa bidhaa hiyo, ihakikishe hakuna malalamiko kama msimu iliyopita ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa wingi na nchi kuwa na chakula cha kutosha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Moshi Lusonzo

# Turekebishe makosa uchaguzi wa mitaa

**WAKATI** uchaguzi wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika mwishoni mwa mwezi huu, Novembа 27, lakini vilio vya kuenguliwa kwa wagombea katika kinyang'anyiro hicho vinasikika kila kona.

Idadi kubwa ya wagombea hao ni kutoka vyama vikuu vya upinzani vya CHADEMA, ACT-Wazalendo na CUF ambao walijaza fomu katika ngazi ya mitaa, vijiji na vitongoji.

ACT Wazalendo, inaripoti kuwa asilimia 60 ya wagombea wake wameenguliwa, huku CHADEMA ikilalamika wagombea 242 wameondolewa katika wilaya ya Kilosa na wengine kadhaa katika mikoa tofauti.

Kwa mujibu wa ratiba ya uchaguzi, Novemba 8, ilikuwa ni siku ya uteuzi wa wagombea waliojitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Hata hivyo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, anavikumbusha vyama vya siasa, wagombea na wadau wengine wa uchaguzi kuwa asiyeridhika na taratibu za uchaguzi akate rufani.

Pamoja na kauli hiyo ya kutia moyo ya Mchengerwa, bado songombingo zilionekana kuongezeka kwa maofisa wa uchaguzi kudaiwa kufunga ofisi na hivyo rufaa hizo kukwamishwa.

Wakati hali hiyo ikiibua vilio kila kona, kuna hoja za msingi zimejitokeza kiasi kwamba zinaonyesha wasiwasi wa kuwepo na ombwe au upungufu katika maandalizi na uratibu wa uchaguzi wa serikali za mitaa nchini.

Kuanzia vyama vya siasa vyenyewe vinatakiwa kujitafakari kwa kina njia vinavyotumia kupata wagombea wake, kwani kuwa wasiwasi vyama vingi vya siasa havina utaratibu bora wa kuwaandaa na kuwateua wagombea ili kwenda kushindana.

Kutokana na makosa ambayo yanadaiwa kujitokeza na hatimaye kuondolewa kwa wagombea hao, inaelezwa wengi wao hawakujaza kama inavyotakiwa fomu za wagombea na wengine kushindwa hata kutaja umri wao. Kutokana na makosa hayo madogo.

Kama vyama vya siasa vingekuwa na maandalizi mazuri yasingejitokeza kwani yangesahihishwa na vyama husika kabla ya kupelekwa kwa ofisi za uchaguzi kwa ajili ya kupitiwa.

Lakini hayo hayakufanyika, kinachoonekana hapo baada ya kupitishwa katika mchujo, wagombea hao walikwenda kuchukua fomu na kuzijaza bila usimamizi wa vyama husika na hatimaye kuzalisha wimbi hilo la wagombea kutokubaliwa kwa kukosa sifa.

Utaratibu huo wa wagombea kujaza fomu bila usimamizi wa vyama husika, sio wa leo wala wa jana, kwani kila uchaguzi unapotokea manung'uniko hayo hujitokeza na kusababisha taharuki miongoni mwa wadau wa siasa hapa nchini.

Viongozi wa vyama vya siasa watambue asilimia zaidi ya 90 ya wanachama wao hawana uelewa mpana kuhusu kanuni za uchaguzi, hivyo ni muhimu kutoa elimu ya chaguzi kabla na baada ya kuwapata wagombea ili iwe rahisi kuondokana na makosa kama hayo.

Kwa kueleza hivyo, sio kwamba kuondolewa kwao ni halali, la hasha, bali ni kujaribu kuondokana na visingizio ambavyo vinaweza kutumika kwa ajili ya kuwanyima haki yao.

Kuhusu TAMISEMI inayosimamia uchaguzi huo, ni muhimu isimame kama mlezi na msimamia haki zaidi, kukuza na kuimarisha demokrasia katika uchaguzi wa serikali za mitaa, badala ya kuendeleza sintofahamu.

Kuyaondoa majina kwa makosa madogo kama kukosea herufi ya jina, ambayo Rais Samia Suluhu Hassan, alikataa haipaswi kuwa ni moja ya vigezo vya kukosa sifa.

Itumike njia bora zaidi ya kuwaelemisha na kuyaona makosa kama hayo ni ya kibinadamu na si jambo la kuongeza mpasuko kwenye uchaguzi.

Malalamiko kama hayo yakizidi kuendelea yanaweza kuweka nchi katika nafasi mbaya ya watu kukosa usawa wa haki zao za msingi za kuchagua au kuchaguliwa. Tamko la Waziri Mchengerwa limekuja kwa wakati katika kurekebisha suala hilo, lakini hilo halitoshi kwani kuwaagiza maofisa kuzifanyia kazi rufaa hizo kwa uhalidilifu na kuwarudisha wale waliondolewa kimakosa ni hatua inayosubiriwa na wengi.

Watanzania wanategemea Waziri Mchengerwa atasimamia vyema uchaguzi wa mitaa na itakuwa moja ya mtihani wake mkubwa katika nafasi yake ndani ya serikali ya awamu ya sita, hivyo asiondoe imani hiyo.

# Aliyeshinda kura za maoni CCM aeleza siri

**Na Julieth Mkireri,** VIGWAZA

MSHINDI wa kura za maoni kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kitongoji cha Kwakisali, Kijiji cha Kwazoka, Halmashauri ya Chalinze, Zena Mkanga, amesema wananchi wanachohitaji ni maendeleo kutoka kwa viongozi wao bila kujali ni kiongozi wa jinsi gani.

Zena ameyasema hayo alipokuwa akizungumza na Nipashe jana kuwa kiongozi yeyote anaweza kuongoza endapo tu atakuwa na uwezo wa kuwaunganisha wananchi na kushirikiana kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema wapo wanawake wenye uwezo wa kuongoza, lakini wanakwamishwa na woga na kushindwa kuthubutu kuingia kwenye kinyang'anyiro kwa kuhofia wagombea wanaume.

"Mimi hii ni mara yangu ya pili nashinda kura za maoni nasubiri tu upande wa wananchi wote, nilishaacha uwoga ninachofanya ni kujenga ushirikiano na wananchi wangu kutatua vikwazo kwenye eneo langu la uongozi," alisema.

Alisema unyanyasaji wa kijinsia unatakiwa kupingwa kwa kwa kuwa ni sababu ya baadhi ya wagombea kushindwa kuchukua fomu hata ndani ya vyama vyao.

"Unaweza ukachukua fomu unagombea na wanaume wengi ili kukudhoofisha, wanaanza kusema upungufu wako, sasa ukiwa mwoga huwezi kumudu kupambana nao watakudhoofisha na utaachana na unachogombea tusikatishwe tamaa na hili kundi tujiamini wenyewe," alisema.

Zena aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti Kijiji cha Kwazoka, alisema alishindwa kwenye kura za maoni na baadaye akaenda ngazi ya kitongoji na wanachama walimpa nafasi.

Naye Mwantumu Rajabu, aliyekuwa mgombea pekee kura za maoni CCM katika kitongoji cha Kambini, Kata ya Vigwaza, alisema wanachama walimpa nafasi hiyo kutokana na aliyoyafanya katika awamu iliyopita.

Wagombea nafasi ya wenyeviti ngazi ya vitongoji kutoka CCM wanawake 14 kati ya vitongoji 53 kwenye kata hiyo wanatarajiwa kuchuana na wagombea wengine kutoka vyama vingine vya siasa kuwania nafasi hiyo Novemba 27.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Salim Msangi, akiwasilisha taarifa ya utendaji ya TCAA katika Mkutano wa 8 wa Jukwaa la Wahariri uliofanyika jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: DICKSON MULASHANI**

## KESI YA KUCHOMA MKE

# Mahakama yapokea udongo wenye masalia ya mafuta

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imepokea udongo wenye masalia ya mafuta yanayodhaniwa kuwa ni ya marehemu Naomi Marijani, ambaye mwili wake ulichomwa moto kwa magunia mawili ya mkaa na mume wake Khamis Luwongo (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe.

Aidha, mmoja wa ndugu wa marehemu (mwanamke), alishindwa kujizuia na kuangua kilio mahakamani na kutoka nje baada ya mahakama kuruhusu udongo huo wa kilo kama 20 uliyokuwa kwenye kiroba ufunguliwe.

Kielelezo hicho namba nane cha upande wa mashtaka kilipokewa jana na Jaji Hamidu Mwanga anayesikiliza kesi hiyo, baada ya kutupilia mbali pingamizi la jopo la mawakili wanne wa mshtakiwa la kupinga udongo huo usipokewe kama kielelezo.

Mahakama ilifikia uamuzi huo, baada ya shahidi namba 12 wa upande wa mashtaka Hadija Mwema (47) ambaye ni Mkemia kutoka Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kuiomba Mahakama ipokee udongo huo kama kielelezo.

Shahidi huyo alifungua udongo huo saa 5:43 asubuhi ndani ya kizimba cha mahakama huku akisaidiwa na askari polisi wawili na kisha kuuchota kwenye kiganja chake na kuionesha Mahakama masalia hayo na kwenye mikono yake alivaa gloves na kuziba mdomo wake kwa barakoa.

Hata hivyo, mmoja wa mawakili wa mshtakiwa Mohamed Majaliwa, alipinga kielelezo hicho kupokewa kwa madai kuwa hakipo katika orodha ya vielelezo toka awali.

Akijibu hoja hiyo, Wakili wa Serikali Mwandamizi Mwasiti Athuman, ambaye alikuwa akimwongoza shahidi, alidai kielelezo hicho kipo kwenye maelezo ya awali (PH) ukurasa wa saba.

Wakili Majaliwa alidai hawana pingamizi na udongo, kwenye PH imeandikwa kwamba ni mabaki ya mwili wa marehemu, udongo sio mabaki, mabaki ni kama meno na mifupa. Mwema aliendelea kusisitiza kwamba udongo huo ni masalia kama alivyoeleza.

Hata hivyo, Majaliwa aliendelea kupinga kwamba mabaki na udongo ni vitu viwili tofauti na pia Mwasiti aliendelea kutetea hoja yake kwamba kwenye ukurasa wa saba hicho kielelezo kipo.

Jaji Mwanga alimtaka Shahidi Mwema asaidie katika hilo kama mtaalamu kwamba humo ndani ya huo udongo kuna nini? Shahidi alidai ni udongo wenye masalia ya mafuta ya binadamu.

Jaji Mwanga alimuuliza Wakili Majaliwa, kama mafuta ni mabaki au la, akajibu kwamba sio mabaki, "Ukiniambia udongo ni masalia wananichanganya," alidai Majaliwa.

Jaji alimtaka Wakili Mwasiti amsomee PH kipengele alichokitaja mahakamani, alikisoma tena kwa mara ya pili, jaji alitaka udongo huo ufunguliwa kwa ukubwa.

Saa 6:02 mchana, Jaji Mwanga alishuka kutoka kwenye kiti chake akiwa amevaa gloves mikononi na kwenda hadi kwenye kizimba alichokuwapo shahidi na kuanza kuangalia kwa karibu udongo huo.

Saa 6:04 mchana Jaji Mwanga alirudi kwenye kiti chake, na kumuuliza Wakili Majaliwa kama anataka kuweka pingamizi hilo, naye alijibu ndiyo na mahakama ikamtaka aanze kuwasilisha pingamizi lake.

"Pingamizi letu ni udongo unaodhaniwa ambao sio miongoni mwa vielelezo ambavyo wenzetu walivyosema wanavitoa, wameleta tu bila notes na kifungu namba 289 (1) (2)(3)(4) cha CPA vikisomwa pamoja vinaeleza wazi walitakiwa wafanye nini," alidai Wakili Majaliwa.

Akijibu hoja hiyo, Wakili Mwasiti alidai kuwa kielelezo hicho kilitajwa toka awali wakati kesi hiyo inaandaliwa kusikilizwa, kilitajwa kama kielelezo namba nane na kwamba sio kweli kwamba wamewashtukiza ni kitu ambacho kilikuwapo, sio kigeni.


Saa 6:19 mchana Jaji Mwanga alitoa uamuzi kuwa amesikia hoja za pande zote mbili na anatupilia mbali pingamizi la upande wa utetezi, kwamba hakuna tafsiri ionekane mifupa tu ndiyo mabaki ya binadamu, na haoni kama kuna kitu cha kushtukiza.

"Mahakama inatupilia mbali pingamizi hili, napokea kama kielelezo P8," alisema Jaji Mwanga.

Mshtakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni, alimuua Naomi Marijani.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Kamati ya Bunge yataka watumiaji Daraja la Nyerere kulipia kwa bando

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imeridhishwa na utaratibu wa ununuzi wa bando la tozo kwa matumizi ya Daraja la Nyerere, Kigamboni na kuwataka watumiaji wa daraja hilo kulipia bando kwa kuwa ni nafuu, rahisi na linapunguza msongamano na kuongeza mapato.

Akizungumza wakati wa majumuisho ya ziara ya kamati hiyo, juzi ilipotembelea miradi ya NSSF ukiwamo wa daraja hilo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Toufiq, amepongeza kazi kubwa inayofanywa na NSSF katika daraja hilo hususan ya kuweka matumizi ya bando.

"Tunaendelea kuipongeza serikali na wenzetu wa NSSF kwa kazi nzuri sana ambayo imefanyika pale Daraja la Nyerere kiukweli kumewekwa mifumo mizuri ambayo licha ya kupunguza changamoto ya foleni, lakini pia inapunguza mianya ya upotevu wa mapato," alisema Fatma.

Alisema Kamati pia inamshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa namna anavyoleta maendeleo nchini kwa manufaa ya wananchi na kuwa wanaunga mkono juhudi zote zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita na kuwa wanaamini mifuko ya hifadhi ya jamii ukiwamo wa NSSF utaendelea kuleta tija kwa wanachama kupitia uwekezaji unaofanywa na mifuko hiyo.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo akiwamo Katani Katani, amepongeza mfumo wa ununuzi wa bando katika daraja hilo na kuwataka wananchi kujiunga kwa kuwa ni rahisi na rafiki na pia unaondoa foleni.

Naye Mariam Kisangi alisema mradi wa Daraja la Nyerere umechochea maendeleo ya wananchi wa Kigamboni na kuwataka kuendelea kulipia tozo za kupita kwa kutumia bando kwa kuwa inapunguza usumbufu.

Athumani Maige aliwataka wananchi kuendelea kutumia matumizi ya bando wakati wanapopita katika daraja hilo na pia ameipongeza NSSF kwa usimamizi mzuri wa mradi huo.

Awali, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, alisisitiza elimu iendelee kutolewa kwa wananchi na watumiaji wa daraja kutumia malipo ya bando kwa kuwa ni rahisi na inapunguza usumbufu.

"Matumizi ya bando ni mazuri na yataongeza mapato, kupunguza kero kwa watumiaji wa daraja hivyo ni muhimu wananchi kupewa elimu zaidi ili watumie bando kuondoa usumbufu," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, amesema wanaendelea kuwahamasisha watumiaji wa daraja kulipia bando la siku, wiki au mwezi ili waweze kupita kwa urahisi hasa ikizingatiwa kuwa matumizi ya bando ni nafuu zaidi.

Mshomba aliipongeza kamati hiyo na kuahidi kuwa maoni, maelekezo na ushauri uliotolewa na wajumbe wa kamati hiyo watauafanyia kazi kwa ajili ya utekelezaji.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Ridhiwani Kikwete, akihamasisha dereva wa pikipiki kutumia bando wakati anapopita Daraja la Nyerere Kigamboni wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, iliyotembelea mradi wa daraja hilo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Kesi ya wizi mamilioni kuanza kusikilizwa Des. 17

**Na Mwandishi Wetu**

KESI ya wizi wa mali mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 600 na Dola za Kimarekani 1,750 inayomkabili mfanyabiashara Christopher Msuya na anayedaiwa kuwa baunsa Kuhani Musa na mwenzake, imepangwa kuanza kusikilizwa ushahidi wa Jamhuri Desemba 17, mwaka huu.

Mshtakiwa wa kwanza katika kesi hiyo ni Reuben Mwaikinda (49).

Washtakiwa hao walisomewa maelezo ya awali juzi mbele ya Hakimu Mkazi Nabwike Mbaba.

Wakili wa Serikali, Vaileth David, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na upande wa Jamhuri uko tayari kuwasomea washtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Mbaba aliridhia ombi la Jamhuri. Wakili Vaileth alidai kuwa katika shtaka la kwanza linalomkabili mshtakiwa wa pili Msuya, anadaiwa kuwa Novemba 25, 2023 eneo la Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam, aliiba vitu mbalimbali vyote vikiwa na thamani ya Sh. 614.113,000 na Dola 1,750 mali ya Theophrida Mhagama.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa siku na eneo la tukio mshtakiwa wa kwanza Mwaikinda Edmond Ngemela, anadaiwa kumsaidia Msuya kutenda kosa la wizi wa mali za mlalamikaji.

Washtakiwa waliposomewa maelezo ya awali walikiri anwani zao na kumfahamu mlalamikaji.

Washtakiwa kwa nyakati tofauti walikana kuwapo Mbezi Beach eneo la Kilongawima na kukana kutenda mashtaka yote mawili.

Wakili Vaileth alidai kuwa upande wa Jamhuri unatarajiwa kuita mashahidi saba na vielelezo vinne kuthibitisha makosa dhidi ya washtakiwa.

Hakimu Mbaba alisema kesi hiyo itaanza kusikilizwa ushahidi Desemba 17, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kuwa nje kwa dhamana.

# MUHAS yaanza kuwanoa wanafunzi sekondari

**Na Grace Mwakalinga**

CHUO Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), kimeanza kuwajengea uwezo wanafunzi wa kike katika shule mbalimbali za sekondari jijini Dar es Salaam na wanawake namna ya kutumia dijitali na uvumbuzi katika masuala ya afya.

Wameamua kuyajengea uwezo makundi hayo baada ya kuona idadi ndogo ya ushiriki katika matumizi ya teknolojia na uvumbuzi katika sekta ya afya.

Naibu Makamu Mkuu wa MUHAS, Profesa Emmanuel Balandya, juzi katika kongamano la nne la wiki katika masuala ya dijitali kwenye sekta ya afya, lililofanyika chuoni hapo alisema katika utafiti waliofanya waliona ushiriki mdogo wa wanawake na mabinti katika matumizi ya teknolojia.

Prof. Balandya alisema kongamano hilo lilianza mwaka 2021 na kwa sasa ni mara ya nne kufanyika na linasaidia kuboresha mifumo ya dijitali kusomana katika kila sekta.

"Tumeona kuwa kidogo cha matumizi ya dijitali katika sekta ya afya na ili tunafanikiwe na kufika mbali lazima tuanze kuwatengeneza wataalamu kuanzia chini na hapa ni watoto wetu hususani wa kike ambao hushiriki wao katika masomo ya Sayansi ni mdogo, kupitia mkakati huu tuwasaidie kuongeza idadi na kulisaidia taifa kuwa na wataalamu watoasaidia mifumo hiyo," alisema Prof. Balandya.

Aidha, alisema MUHAS wanataka mifumo yote ya kisekta isomane, ili kurahisisha utoaji wa huduma ikiwamo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Afya.

"Katika sekta ya afya bado hatufanyi vizuri katika suala la utunzaji na utoaji wa taarifa aidha za wagonjwa na kumbukumbu nyingine, tunahitaji kushughulikia suala hili, kusaidia utunzaji wa taarifa kidigitali badala ya kuhifadhiwa kwenye vitabu," alisema.

Alisema wataendelea kuzalisha wataalamu kwa ajili ya kusaidia kuingiza mifumo yote inayotoa huduma za kijamii kusomana kidijitali kwa kuzingatia miongozo ya serikali.

Akifungua kongamano hilo kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Carolyne Nombo, Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Ufundi, Idara ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Dk. Mwajuma Lingwanda, alisema ushiriki wa mabinti na wanawake kwenye matumizi ya kidijitali itaziba pengo lililopo la idadi yao ndogo ya ushiriki.

Dk. Mwajuma alisema kama lengo la kongamano hilo linavyojieleza kuziba pengo na uunganisha wanawake na mabinti katika matumizi ya dijitali.

Aidha, alisema kushinda vizuizi hivyo ni muhimu kusikiliza sauti za wanawake na mabinti na kuelewa changamoto zao maalum na fursa zilizopo, watafiti wa MUHAS, mtusaidie kushughulikia ili kusaidia wanawake na mabinti kung'ara katika mageuzi ya sekta ya afya kidijitali.

Aliongeza kuwa wizara, imedhamiria kutekeleza maono hayo, kuendelea kukuza elimu ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, na Hisabati (STEM) kwa wasichana, kuongeza upatikanaji wa rasilimali za kidijitali na kujenga majukwaa yatakayohamasisha ubunifu na uongozi miongoni mwa wanawake.

Debora Enock, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mbezi Inn, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa kuwa yatawasaidia kujua ni kwa namna gani watatumia dijitali kupata taarifa katika sekta ya afya.

Kalyne Mseki, mwanafunzi wa kidato cha sita Shule ya Sekondari Jangwani, alisema katika kuhakikisha kuna idadi kubwa ya wasichana na katika matumizi ya dijitali ni muhimu serikali kwa kushirikiana na wadau wakawekeza kwenye ununuzi wa vifaa shuleni.

Alisema hatua hiyo itasaidia wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kujua namna masuala ya teknolojia yanavyofanya kazi na kuwahamasisha kutumia maarifa hayo hata wanapohitimu shule.

HABARI KASKAZINI

## CHADEMA yawapongeza wasimamizi uchaguzi

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, kimewapa 'kongole' kwa mara ya kwanza, wasimamizi wa uchaguzi kwa kutenda haki na kuwapitisha wagombea wao wote.

Katibu Mwenezi wa CHADEMA, Wilaya ya Simanjiro, Ambrose Ndege, ameeleza kuwa wanatarajia kuanza kufanya kampeni ya uchaguzi Novemba 20 kwenye maeneo mbalimbali.

"Tunawashukuru viongozi wa Wilaya Simanjiro na kata zote na za kata za Mji Mdogo wa Mirerani kwa kutenda haki bila kubagua au kukata majina ya wagombea wetu," alisema Ndege.

Aliishukuru TAMISEMI (Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), kwa kuweka viongozi makini Wilaya ya Simanjiro, kata zote na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, kwani wamesimamia mchakato wa uchaguzi vyema na sasa wanasubiria kuanza kampeni muda utakapofika.

"Wagombea wote kwenye maeneo tuliyowasimamisha wamepitishwa hakukuwa na vikwazo vya fomu kukosewa au mizengwe yoyote tumetendewa haki, watu waingie uwanjani wanadi sera zao wapigiwe kura na siyo kupita bila kupingwa," alisema Ndege.

"Tangu mwaka 2014 hatujafanya uchaguzi wa halali Simanjiro, kwani wagombea wetu wamekuwa wakienguliwa ila mwaka huu wa 2024 tunawapongeza viongozi wa serikali kwa kutekeleza vyema wajibu wao," alisema Ndege.

Alisema kwenye Mji Mdogo wa Mirerani, wamefanikiwa kusimamisha wagombea uenyekiti kwenye vitongoji 23 kasoro kitongoji kimoja.

"Huyu mgombea wa Zaire ameandika barua mwenyewe ya kutogombea ila hakukatwa jina lake ameamua mwenyewe hatufahamu kilichomsibu," alisema Ndege.

Mwanachama wa CHADEMA, Adam Woisso, alisema wasimamizi wa uchaguzi wamefanya vyema, kwani jamii inapaswa kufanya uchaguzi kwa kuchagua wagombea, kupitia vyama na siyo kuwapitisha bila kupingwa.

Alisema: "Kwa hapa wasimamizi wa uchaguzi wanastahili pongezi, kwani wametekeleza wajibu wao ipasavyo na sisi tunajipanga vyema, kwenye maandalizi ya kufanya kampeni".

**Alisema kwenye Mji Mdogo wa Mirerani, wamefanikiwa kusimamisha wagombea uenyekiti kwenye vitongoji 23 kasoro kitongoji kimoja.**

# TAKUKURU yabaini tatizo mitambo kufua umeme

**Na Mary Mosha,** MOSHI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imebaini mitambo miwili ya kufua umeme, iliyonunuliwa na Kampuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KADCO) ili kuzalisha umeme wa dharura, injini zake ni za zamani.

Mitambo hiyo imenunuliwa kutoka Kampuni ya African Power Machinery (APM) kwa gharama ya Sh. 3,294,796.

Jana Naibu Mkuu wa TAKUKURU, Mkoa wa Kilimanjaro, Stella Saleh, alisema matokeo ya ufuatiliaji wa miradi ilibaini KADCO kufanya manunuzi ya jenereta mbili zilizowasilishwa zilikuwa na mapungufu kadhaa ikiwa ni pamoja na kebo zilizotakiwa kuwa tofauti na zilizowasilishwa.

Matokeo hayo ya ufuatiliaji yamo katika ripoti ya robo ya kwanza ya mwaka 2024/25 yaani Julai hadi Septemba mwaka huu.

Aidha, alisema injini za jenereta hizo zilikuwa za zamani na baadhi ya maeneo ya mitambo hiyo ilikuwa na kutu na maeneo mengine yalikuwa yamepakwa rangi.

"TAKUKURU Wilaya ya Hai, ilifanya udhibiti juu ya ununuzi wa jenereta hizo mbili na kuzuia malipo kufanyika kwa kampuni iliyosambaza, na kuokoa fedha hizo, ambazo zingetumika kulipia jenereta zisizo na ubora kulingana na mahitaji yaliyoainishwa," alisema.

Katika hatua nyingine, TAKUKURU imebaini kusuasua kwa ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Moshi kutokana na kutofanyika malipo kwa wakati kwa mkandarasi Humphrey Construction Co.Ltd ya Sh. milioni 213.6.

Alisema: "Tulifuatilia na mnamo Agosti 10 mwaka huu, aliweza kulipwa na ujenzi kuendelea."



Wakazi wa Kitongoji cha Chang'ombe, Kijiji cha Enguserosidan, Kata ya Laiseri mkoani Manyara, wakimpokea Mbunge wa Jimbo la Kiteto, Edward Ole Lekaita, alipofanya ziara yake kwenye kitongoji hicho juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Mgawo wa maji wawaibua wanawake Kata ya Biriri

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

MAKALI ya mgawo wa maji yamewaibua wanawake wa vijiji viwili vya Naibili na Majengo vilivyoko Kata ya Biriri, Wilaya ya Siha kupaza sauti wakitaka hatua za haraka zichukuliwe.

Kiongozi wa jopo la wana vikundi vya wanawake, Mary Manjano, alisema wamelazimika kuwaita mbele yao, Meneja wa Mradi wa Maji wa Magadini/Makiwaru Water Supply na Bodi yake, pamoja na Meneja wa Mradi wa Lawate/Fuka Water Supply ili kujibu hoja zao na kutatua tatizo hilo.

Manjano alikuwa aliwasilisha ajenda nne za wanawake hao katika mkutano maalum wa utatuzi wa kero uliofanyika Kijiji cha Naibili.

"Sisi kama wanawake, tumekutana na changamoto kubwa sana ya kukatika maji mara kwa mara, lakini pia maji kutoka machafu.

"Hali hii imekuwa ikisababisha sisi wanajamii na hasa wanawake kupata shida; wakati mwingine tunaletewa tangazo la kulipa ankara za maji lakini wenye mamlaka hawazungumzii tatizo la kukatika maji mara kwa mara.

Zaidi alifafanua: "Tumepata majibu tumeridhika na wametuahidi kwamba yako ambayo wataenda kuyafanyia kazi, tumerudishiwa imani."

Mkazi wa Kijiji cha Majengo, Ruwaichi Shirima, alisema lengo lao ni kuona malengo yao tarajiwa waliyokuwa wanayataka yametimia. Kwamba, mwanamke sasa lile tatizo la kwenda kuchota maji umbali mrefu linapungua lakini pia na maji yanatibiwa.

Akijibu hoja za wananchi hao, Meneja wa Mradi wa Maji wa Magadini/Makiwaru Water Supply, Ezekiel Maingo, alisema amepokea malalamiko hayo na ofisi yake itachukua hatua za haraka kutatua changamoto zilizotajwa na kuhakikisha vijiji hivyo na vitongoji vyake, vinapata huduma hiyo kwa wakati.

Kuhusu changamoto za afya, wananchi wa vijiji hivyo, wameeleza namna wanajamii wanavyokabiliwa na changamoto ya bima za wazee kutofanya kazi.

Augenia Massawe alisema, "Mzee anapokwenda pale hospitali, kwa sababu amekata bima yake hapati zile huduma mpaka awe na fedha. Pale Hospitali ya Wilaya, dawa hazipatikani, lakini nje ya hospitali unakuta kuna duka la dawa.

Katika mkutano huo, Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Naibili (VEO), Melchiory Moiti, alilishukuru Shirika la kiraia la TUSONGE CDO, kwa kuwa mkono wa pili wa serikali, likitoa elimu kwa wanawake, hasa uwekezaji katika vikundi vya kiuchumi kama vikoba, utunzaji wa fedha na uanzishwaji wa miradi ya kiuchumi.

"Kupitia TUSONGE CDO, jamii yetu imepona kutokana na kupata elimu ya uhifadhi wa mazingira, suala la ukatili, hususani mimba za utotoni, vipigo na ukatili wa kingono. Changamoto hizo sasa zimekuwa zikitatuliwa kirahisi kuliko ambavyo sisi tungetatua wenyewe."

Tunamshukuru Mungu kwa Shirika la TUSONGE kutupa mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, kilimo na elimu ya kujitambua, ambayo imetufanya sisi kama wanawake kutambua haki zetu kimsingi lakini na kuzichakata na kuona ni wapi tuwasilishe hoja zetu.

Ofisa Ufuatiliaji na Tathmini wa Tusonge CDO, Gilbert Owen, akizungumza katika mkutano huo, aliipongeza serikali akisema imekuwa ikifanya vizuri kuchukua hatua katika kila jambo linaloibuliwa na wananchi wa kata hiyo.

# Asimulia alivyonusurika kuozwa mahari ya 200,000/-

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kijiji cha Nyikoboko mkoani Shinyanga, Kashinje Mwendesha (20), ameeleza namna alivyonusurika kuozeshwa na wazazi kwa mahari ya ng'ombe saba na Sh.200,000 baada ya kuhitimu elimu ya sekondari.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kashinje alieleza kuwa alifikwa na mkasa huo mwaka 2020 akiwa na ufaulu wa daraja la pili, alifanikiwa kukimbia njama hizo zilizopangwa na wazazi wake.

Alisema alifanikiwa kuendelea na masomo na sasa anasoma Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) fani ya maendeleo ya jamii.

Kashinje aliiambia Nipashe kuwa safari yake ya kutaka kuozeshwa ilianza alipohitimu kidato cha nne Sekondari ya Nyikoboko.

Alisema wakati akisubiria matokeo wachumba walianza kujitokeza na kufanya mazungumzo na wazazi wake.

Kahinje alisema, wiki mbili baadaye alijitokeza mchumba mwingine na kuzungumza na wazazi wake ambaye alikubali kutoa mahari ya ng'ombe hao na kiasi cha fedha na hapo ndipo mama yake mzazi alipomtaka kuolewa akisema hawako tayari kuacha kupokea mahari hizo.

"Mimi sikutaka kuolewa kabisa, familia nzima ilinichukia kwa kukataa kuolewa na nilikosa amani kwa kuwa kila mmoja alikuwa ananiona mbaya na mwenye kuwapinga wazazi wangu ambao wanaiona kesho yangu," alisema Kashinje.

Alisema majirani nao walimshawishi kukubali kuolewa, lakini alichukua uamuzi wa kutoroka na kwenda kwa mjomba wake aliyekuwa anaishi Kata ya Lunguya.

Alisema alipofika kwa mjomba wake alimweleza mkasa mzima lakini naye alikubali aolewa na kuachana na masuala ya kusoma.

Alisema, mwalimu wa sekondari aliyokuwa akisoma, Boniphace Madurya alipopata taarifa hizo alikwenda kuripoti katika vyombo vya sheria na mama yake alikamatwa na kupelekwa kituo cha polisi.



Wagombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Manispaa ya Shinyanga, wakiwa na fomu ambazo wamezijaza kwa ajili ya kukata rufani kufuatia majina yao kuenguliwa kutogombea kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Novemba 27, mwaka huu. **PICHA: MARCO MADUHU**

# MUWASA yawaondoa hofu wananchi utekelezaji mradi

**Na Timothy Itembe,** TARIME

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Musoma (MUWASA) imeawaondoa hofu wananchi wilayani Tarime kuhusu utekelezaji wa mradi wa maji utakaomaliza kero ya upatikanaji maji wilayani humo.

Meneja Kanda ya Tarime, Boniface Kasinde alisema hayo juzi na wakati akijibu hoja za madiwani, kueleza kuwa hadi sasa mradi huo umefikia asilimia 62.2.

Alisema katika kumaliza adha ya maji kwa kanda hiyo waliandaa mpango wa kuboresha ubora wa maji kupitia chanzo cha chemchemu ya Nyandurumo ambako usanifu na tathmini ya kujenga mfumo wa kuchuja maji pamoja na ujenzi umekamilika.

Alisema kuwa kibali cha ujenzi wa mtambo mdogo wa kuondoa tope kilisha tolewa.

Kasinde alisema gharama za utekelezaji wa mradi huo ni zaidi ya Sh. milioni 677.36 na fedha iliyopokelewa mpaka sasa ni zaidi ya Sh. milioni 271.55, huku ukitarajiwa kukamilika mwezi Juni 2025.

Diwani wa Kata ya Turwa, Chacha Machugu alisema katika kata yake kuna mradi wa Gimenya wenye thamani ya Sh. milioni 180, hivyo kuomba wataalamu kuboresha mradi huo ili kutoa huduma zaidi kwa wananchi tofauti na ilivyo kwa sasa.

Mkurugenzi wa Mji wa Tarime, Gimbana Ntavyo, alisema hapo awali kulikuwapo na changamoto ya upatikanaji wa maji katika Shule ya Sekondari Tarime pamoja na Taasisi ya Hospitali ya Bomani.

Alisema lakini kwa kushirikiana na MUWASA taasisi hizo zimepata majisafi kupitia visima virefu wakati wakisubiri utekelezaji wa mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Richard Ngowele, alisema wataalamu wa mamlaka za maji waendelee kusimamia vyema kutoa huduma safi kwa wananchi na kutatua changamoto kadri zinavyojitokeza.

## Wanafunzi Sekondari Sirari wasaidia wagonjwa

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

WANAFUNZI wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Sirari wilayani Tarime mkoani Mara, wamechanga Sh. 800,000 na kuziwakilisha kwa wagonjwa wenye uhitaji katika Kituo cha Afya Sirari.

Akikabidhi msaada wa vyakula pamoja na vifaa vya matumizi ya kawaida kwa wagonjwa vilivyonunuliwa kwa fedha hizo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Sirari, Bulogo Mbeba, aliisihi jamii kuweka utaratibu wa kutoa msaada kwa wasiojiweza ili kuwasaidia kumudu mahitaji yao.

Mbeba alisema watahiniwa hao chini ya viongozi wao wa wanafunzi walianzisha wazo hilo kama ishara ya matendo ya huruma katika jamii inayowazunguka kabla ya kuhitimu masomo yao.

"Wanafunzi hawa zaidi ya 200 walionesha ishara nzuri na kuleta katika utawala mapendekezo yao wenyewe kurudisha upendo katika jamii inayozunguka shule kabla ya kufanya mtihani wao wa mwisho na tukawaunga mkono moja kwa moja," alisema.

Alibainisha kuwa vifaa hivyo kuwa ni pamoja na vyakula kwa ajili ya wagonjwa, sabuni, taulo za watoto wachanga sanjari na kusaidia shughuli za usafi wa ndani na mazingira katika kituo hicho cha afya.

Akipokea msaada huo, Muuguzi Mfawidhi wa kituo hicho, Happiness Tunya aliwashukuru wanafunzi hao kwa hatua hiyo na kuwaasa wanajamii wengine kuiga mfano huo kwa kuwa mahitaji ya wagonjwa hayajitoshelezi.


Alisema: "Hatua iliyochukuliwa na vijana hao ambao wengi wanategemea kupata mahitaji yao ya kila siku kutoka kwa wazazi wao na walezi wao ni ya kupongezwa na inapaswa kuigwa na watu wote katika jamii na kwa niaba ya wagonjwa na uongozi wa kituo tunawatakia mtihani mwema."

**Akikabidhi msaada wa vyakula pamoja na vifaa vya matumizi ya kawaida kwa wagonjwa vilivyonunuliwa kwa fedha hizo, Mkuu wa Shule ya Sekondari Sirari, Bulogo Mbeba, aliisihi jamii kuweka utaratibu wa kutoa msaada kwa wasiojiweza ili kuwasaidia kumudu mahitaji yao.**



Ukurasa 12

**Mafuta kuchanganyika na maji chanzo vifo, kuzaliwa viumbe wa ajabu Sudan**




Ukurasa 13

Hili la kuvuna mabilioni bila kazi subirini tena Trump awakemee





Ukurasa 14

**TRUMP NA USHINDI MAREKANI**

**Mwanamama awa kiongozi mkuu ikulu**

## KUELEKEA UCHAGUZI S/MITAA

# Kuenguliwa wapinzani kunavyoibua hofu matukio ya 2019 kujirudia

**Na Mwandishi Wetu**

MCHAKATO wa kuchukua na kurejesha fomu za kuomba uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa, umemalizika ukiwa umeacha maswali kwa vyama vya upinzani na wananchi.

Ni kutokana na kile kinachoelezwa kuwa wagombea wa upinzani wanaenguliwa katika mazingira na sababu ambazo wanadai zinawashangaza.

Wakati waliopitishwa wakielekea kwenye kampeni za uchaguzi huo zinazotarajia kuanza Jumatano ijayo Novemba 20 hadi 26, vyama hivyo vinasema wagombea wao wengi wameenguliwa, majina yao yakiwa hayaonekani.

Kwa sasa vyama hivyo vinaendelea na mchakato wa kukata rufani ili kuhakikisha wanachama wao walioenguliwa kinyemela yanarejeshwa, watumie haki yao ya kikatiba ya kuchaguliwa.

Vyama vinavyolalamika kufanyiwa figisu kwenye kujaza fomu hizo ni CUF, CHADEMA na ACT-Wazalendo ambapo kila kimoja kinafanya juhudi za kurudisha wagombea wao kwenye kinyang'anyiro.

Kutokana na sintofahamu hiyo inayoendelea, baadhi ya wachambuzi na wadau wa siasa wanazungumza na Nipashe kuhusu mchakato huo.

**HUJUMA R4**

Abdulkarim Atiki ni mchambuzi wa siasa ambaye anasema mchezo wa kuengua wagombea wa upinzani ni kama mkakati wa hujuma kwa Rais Samia Suluhu Hassan ili kuyumbusha utekelezaji wa R4.

"Hizo ni hujuma dhidi ya R4 za Rais Samia zinazolenga kuleta umoja wa Watanzania bila kujali itikadi za vyama. Inakuwaje wasimamizi wanakiuka kanuni? Watafakari kwa kina jambo hili," anasema Atiki.



Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya. **PICHA: MTANDAO**

Anakumbusha kuwa Rais anahimiza kuunganisha Watanzania ili kuepuka mazingira yaliyotokea katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019, lakini dalili zinaonekana yatajirudia katika uchaguzi wa mwaka huu.

"Demokrasi inatakiwa kuanzia ngazi ya chini, yaani wananchi katika kijiji wawe huru kuchagua kiongozi ambaye wanamtaka si wawekewe mgombea wasiyemtaka ndicho kinaendelea sasa, hiyo ni dhambi," anasema.

Mchambuzi huyo anasema kasoro ndogo zisipewe uzito hadi kuengua mgombea ambaye wananchi wanamtaka, na kwamba aachwe agombee matokeo yaamuliwe na sanduku la kura.

Atiki anasema Waziri wa TAMISEMI ambaye anasimamia uchaguzi huo aangalie uwezekano wa kusimamia haki kuepuka kutenda kosa hilo ili aruhusu wananchi wapate wagombea wanaowataka.

"Mimi ni muumini wa demokrasia, ninatamani sana ushindi unaotokana na kujenga hoja majukwaani na si ushindi wa mezani ambao tayari umeanza kuonekana. Inatisha shaka kuamini kama kweli wapinzani hawajui kujaza fomu, au fomu wanazopewa wagombea wa CCM ni nyingine na wapinzani nao wanapewa tofauti zinazowashinda kujaza?

**AIBU YA TAIFA**

Mwanaharakati ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Hellen Kijo-Bisimba, anasema kinachoendelea katika mchakato huo ni aibu kwa taifa.

Anasema ni vyema viongozi wajitokeze hadharani na kukomea vitendo vinavyoashiria kuvuruga uchaguzi wa serikali za mitaa ikiwamo kuengua wagombea wengi wa upinzani ili CCM ishinde kirahisi.

"Waziri kutoka hadharani na kuwaambia walioenguliwa kuwa wakate rufani inaonyesha anajua kila kitu kinachoendelea. Kwa nini asilaani vitendo hivyo na kutoa maelekezo?" Anahoji Dk. Hellen.

Dk. Hellen anasema kuwapo maeneo ambayo wasimamizi wasaidizi walifunga ofisi na kuwanyima nafasi wagombea wapinzani na wengine kukataa kupokea fomu zao bila kuchukuliwa hatua, kunaacha maswali.

"Nimeona video moja wazee wakisema kuwa wanashangaa kusikia kuwa majina yao yameandikwa wakitambulishwa kuwa ni chama fulani wakati si kweli. Nani aliandika majina yao katika chama kingine?" anauliza.

Mwanaharakati huyo anasema mchakato huo una kasoro nyingi ambazo anaona ni bora uwanja ungekuwa sawa kwani inaelekea bado wengine hawako tayari kuona upinzani ukiongoza.

"Ifike wakati CCM iwaachie wananchi wachague viongozi wanaowataka. Mimi siamini kama kweli ndani ya upande mmoja ndiko kuna viongozi bora wasiokosea kujaza fomu au wanaojua kuongoza kuliko wengine," anasema.

**NI MAELEKEZO**

Naibu Katibu Mkuu wa CUF Bara, Magdalena Sakaya, anasema wapo baadhi ya watendaji ambao 'rafu' hizo zinawauma wanaamua kusema ukweli kuwa wanachofanya ni kutekeleza maelekezo bila kutaja kuwa ni ya nani.

Anasema wagombea wa CCM hawana hoja badala yake wanategemea kubebwa na maelekezo ambayo yametekelezwa karibu kila kona ya nchi na kusababisha wapinzani wengi kuenguliwa.

INAENDELEA UK. 12

# Mafuta kuchanganyika na maji chanzo vifo, kuzaliwa viumbe wa ajabu Sudan

**Na Mwandishi Wetu**

UTAJIRI wa mafuta licha ya kuonekana neema kwa raia wa Sudan Kusini, sasa umegeuka kuwa chanzo cha vifo na mateso kwa raia maskini wa taifa hilo jipya na changa duniani.

Ni katika jimbo la Unity ambako mafuta yamesambaa ndani ya mito na mabwawa ya maji ya kunywa tatizo likiongezwa na mafuriko.

Serikali na kampuni zinazochimba mafuta nchini humo zinalaumiwa kwa tatizo hilo ambalo limesababisha vifo, ulemavu na watoto kuzaliwa wakiwa na kasoro za kimaumbile kama viungo kuungana.

Jimbo hilo ndilo kubwa Sudan Kusini linalozalisha mafuta mengi na linakumbwa na mafuriko kila wakati wa mvua. Tangu 2019, mvua kubwa zinazonyesha zinasababisha mafuriko na maji kutuama, kuharibu mashamba, makazi vijijini na pia misitu.

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) lilithibitisha kwamba theluthi mbili ya jimbo la Unity ilifunikwa na maji, hadi sasa karibu asilimia 40 ya jimbo hilo liko chini ya maji.

Hata hivyo, mafuta kusambaa na kufikia maeneo yenye maji yamesababisha janga kubwa kiasi ambacho asilimia kubwa ya watu wa eneo hilo wanakunywa maji yaliyochanganyika na mafuta.

Chifu katika eneo hilo, Chilhok Puot, anasema wapo hatarini kutokana na mafuta kutoka kwenye machimbo kusambaa kwenye maji wanayokunywa, kupikia na kunywesha mifugo.

"Maji ni machafu kwa sababu eneo hili lina mafuta ambayo yana kemikali hatarishi," anasema chifu Puot.

Nyatabah, mwanamama kutoka jamii ya wafugaji wanaoishi katikati ya Unity, anasema mtu akinywa maji hayo anapumua kwa nguvu na kukohoa.

"Tunajua ni maji machafu, lakini hatuna mahali pengine popote, tunakufa kwa kiu." Anaeleza Nyatabah.

**SERIKALI LAWAMANI**

Mhandisi wa zamani wa kampuni ya mafuta ya Greater Pioneer Operating Company (GPOC), David Bojo Leju, ameiambia BBC, kuwa mafuriko katika eneo hilo yanabeba mafuta hadi kwenye vyanzo vya maji.



Mafuta yanayochanganyikana na maji katika eneo la Roriak. **PICHA: BBC**



> Inawezekana uchafuzi unaohusiana na mafuta unaweza kuchangia kuongezeka kwa hatari ya kuzaliwa kwa watoto wenye kasoro.

Eneo kubwa la jimbo hilo liko kwenye maji kwa miaka kadhaa baada ya mafuriko ambayo hayajawahi kutokea, na wanasayansi wanasema yamepata nguvu kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

Sudan Kusini ni taifa changa duniani na mojawapo ya nchi maskini zaidi, ambayo serikali inategemea mafuta kupata pato la taifa. Bojo Leju alifanya kazi kwenye kampuni hiyo ambayo ina ubia kati ya kampuni ya mafuta ya Malaysia, India na China, huku serikali ya Sudan Kusini ikimiliki asilimia tano pekee za hisa.

Baada ya bomba kubwa kupasuka miaka mitano iliyopita, Bojo Leju alianza kupiga picha ya madimbwi ya maji yenye mafuta na marundo ya udongo mweusi katika eneo hilo.

Anasema umwagikaji wa mafuta kutoka katika visima vya mafuta na mabomba lilikuwa ni jambo la kawaida na yeye alihusika katika kuondoa udongo uliochafuliwa katika barabara ili usionekane.

Alielezea wasiwasi wake kwa wasimamizi wa kampuni, lakini anasema hatua iliyochukuliwa ni ndogo na hakukuwa na mpango wa kuusafisha udongo huo.

Bojo Leju anasema maji yanayotolewa kutoka ardhini wakati mafuta yanapotolewa, mara nyingi yanakuwa na hidrokaboni na kemikali zingine hatari.

"Swali ni wapi maji hayo yanakwenda?" Anahoji na kuongeza: "Yanakwenda mpaka mtoni, hadi kwenye vyanzo vya maji ambapo watu wanakunywa, mengine kwenye madimbwi ambako watu huvua samaki."

**ATHARI VIUMBEHAI**

Wanakijiji wa Roriak, wanakunywa maji machafu ambayo yanasababisha athari kwao na mifugo.

Wanasema mifugo inazaa ndama ambao hawana vichwa au viungo. Waziri wa Kilimo wa Jimbo la Unity anasema vifo zaidi ya ng'ombe 100,000 vimeripotiwa ndani ya miaka miwili kutokana na mafuriko pamoja na uchafu wa mafuta.

Katika msitu ulio karibu na Roriak, wanaokata miti kutengeneza mkaa wanasema maji yaliyopo ndani ya msitu ni machafu.

Wakimbizi wanaoishi karibu na mji mkuu wa jimbo hilo, Bentiu, inayohifadhi watu 140,000 waliokimbia vita au mafuriko anasema kambi hiyo imezungukwa na maji ya mafuriko.

Wanatumia maji kutoka kwenye kisima ambacho sio salama kwa ajili ya kunywa na kupikia.

Wataalamu wa afya na wanasiasa katika eneo hilo wameambia BBC, kuwa wanaamini uchafuzi wa mazingira na ukosefu wa maji safi unaathiri afya ya umma.

Katika hospitali moja katika mji wa Bentiu, mama amejifungua mtoto aliyeungana na pua na mdomo .

"Inawezekana uchafuzi unaohusiana na mafuta unaweza kuchangia kuongezeka kwa hatari ya kuzaliwa kwa watoto wenye kasoro," anasema Dk. Nicole Deziel, mtaalamu wa afya ya mazingira katika Chuo Kikuu cha Yale.

Uchafuzi wa mazingira ni sababu ya matatizo ya kuzaliwa watoto njiti, maumbile kutokamilika, matatizo ya uzazi na maambukizi mengine.

Mwaka 2014 na 2017, shirika lisilo la kiserikali la Sign of Hope la Ujerumani lilifanya tafiti karibu na maeneo ya uchimbaji mafuta katika Jimbo la Unity na kubaini kiwango kikubwa cha chumvi na metali nzito katika maji karibu na visima vya mafuta.

Pia maji kulionekana viwango vya juu vya kemikali ya risasi na bariamu katika sampuli za nywele za binadamu.

**SERIKALI HAIJALI**

Bojo Leju anasema kuzungumzia mafuta ni kama kugusa moyo wa serikali, kwani unaweza ukapoteza maisha.

Anasema 2020 alifuatwa na mawakili wa Sudan Kusini ambao walitaka kuishtaki serikali kuhusu uchafuzi wa mafuta.

Alikubali kutoa ushahidi, lakini anasema maofisa wa usalama walimzuia, kumpiga kichwani na bastola na kumlazimisha kutia saini hati ya kubatilisha ushahidi wake.

Kwa sasa anaishi nchini Sweden kama mkimbizi wa kisiasa.

Muungano wa mafuta wa GPOC na ofisi ya Rais wa Sudan Kusini hajatoa kauli kuhusu ripoti hiyo ya kisayansi. **BBC**

## Kuenguliwa wapinzani kunavyoibua hofu matukio ya 2019 kujirudia

**INATOKA UK. 11**

"Katika mchakato huu wametafuta sababu wamekosa wakaamua kubadili majina ya watu. Mfano kuna mgombea wetu anaitwa Mohamed Salum, aliteuliwa, lakini baada ya siku chake akapigiwa simu kuwa ameenguliwa kwa sababu amekosea kuandika jina.

Anaambiwa kuwa badala ya Salum ameandika Saluma. Yaani kule mwisho waliongeza herufi 'a'," anasema Magdalena.

Anakumbusha kuwa chama chao kilianza kupiga kelele tangu mchakato wa kuandikisha wapigakura, kuchukua fomu na kurejesha, na kwamba hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

"Kwa kuwa kauli za TAMISEMI zimekuwa ni za kawaida, mimi niwaombe viongozi wakuu wa nchi wajitokeze hadharani na kukemea vitendo hivi ambavyo vinatibua R4 za Rais," anasema.

Aidha, Magdalena anaitaka Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa isiendelee kukaa kimya badala yake iingilie kati kama mlezi wa vyama hivyo ili upinzani usiendelee kulalamika katika mchakato huo.

Wakati kukiwa na sintofahamu, Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa, ameshatoa maelekezo ya kuwataka wagombea walioenguliwa wakate rufani na kwamba zitasikilizwa kwa haki.

JANGA LA KUBETI

# Hili la kuvuna mabilioni bila kazi subirini tena Trump awakemee

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, anadai kuwa Waafrika 'hawajatimia' wana upungufu kuanzia fikra, matendo na kumudu maisha yao.

Wanahitaji kuongozwa na Wazungu zaidi, kwa kuwa wana kila rasilimali lakini hawawezi kupanga wala kujipatia maendeleo. Wanazaliwa maskini na ombaomba hadi kufikia kifo wamebaki fukara.

Inawezekana analosema likapingwa au likachukuliwa kila mmoja kwa mtazamo wake, lakini hili la Afrika kuwa karakana ya kubeti na vijana wake kutegemea kupata pesa nyingi kwa mkupuo bila kufanyakazi msingojee Trump awaambie.

Viongozi wa Afrika wakumbuke kuwa kazi ni nguzo muhimu katika maisha na ndiyo ufunguo wa kila kitu kuanzia mtu binafsi, familia na taifa kupata uchumi na maendeleo endelevu.

Hakuna usawa kwenye jamii pasipo kila mtu kufanya kazi. Mataifa yaliyoendelea ya Ulaya, Asia kama China na Japan, Amerika mfano Marekani na Canada yameweka juhudi nyingi na kuongeza ufanisi kwenye kufanya kazi.

Watu wa jinsia zote watoto, wazee kwa vijana wanajituma kwenye kazi. Leo wanajivunia mafanikio na maendeleo makubwa ambayo Afrika inayoyasikia hata kuyaona.

Linapokuja suala la kazi hali kwa Afrika na Tanzania ni kichekesho. Dunia ya leo watu wanahimizwa kusaka pesa bila kufanya kazi kwa kuhamasishwa kucheza kamari au kubeti. Ndiyo michezo ya kubahatisha.

Katika majiji, mijini na vijijini kamari ndiyo habari mubashara kila mahali ni mabango na matangazo kwenye runinga na redio.


Vijana wanahamasishwa kuwa mmoja akicheza kwa Shilingi kadhaa, mathalani Kenya, Tanzania na Uganda atapata milioni nyingi kuanzia tano,10, 50 na zaidi.

Kwa buku tu unalala maskini unaamka tajiri. Afrika inapohimiza raia wake hasa vijana wasifanye kazi wategemee kubeti au kamari ili wawe matajiri 'imelikoroga'.

Ni muhimu kusema ukweli kuwa ni lazima kufanya kazi ili kupata pesa na hakuna zaidi. Kama ni mfanyakazi wa kuajiriwa atapokea mshahara au ujira mwisho wa mwezi.

Kadhalika, kwenye biashara utapata faida ndiyo pesa unazotaka.

Aidha, unaweza kupata fedha kwa kupewa urithi na mzazi au mlezi na zaidi unajipatia fedha unapokopa kutoka taasisi za fedha au za serikali kama ulivyo mkopo wa halmashauri ukitoa fedha kwa mfumo wa asilimia




4:4:2 kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

Ukweli ni kwamba hakuna mapato halali nje ya kazi halali. Vijana wanaopanga misururu kubeti hawawezi kuondoa umaskini na sio rahisi kutumia 'buku' siku moja ukapata milioni 10 papo hapo.

**UKWELI USEMWE**

Kwa mujibu wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), nguvu kazi ya vijana katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara inatarajiwa kufikia milioni 72.6 kati ya mwaka wa 2023 na 2050.

ILO inasema ukuaji huo unaweza kuandaa fursa ya kuwa na nguvukazi kubwa duniani ya uzalishaji na kubadili sura ya bara hili kutoka kwenye ufukara na kuwa nchi ya asali na maziwa.

Hata hivyo, nchi nyingi za Kiafrika hazitengenezi ajira za kutosha kwa ajili ya vijana, badala yake zinaruhusu kampuni za kubashiri na kubeti au kuendesha pikipiki na kupata ajali zinazowaua vijana hao kila siku.

Afrika ina 'kichaa cha kubeti' na kubashiri matokeo ya mpira wa miguu au 'match fixing'. Kwa upande wa eneo la Kusini ya Sahara Nigeria inaongoza kwa kubeti na kubashiri matokeo ya kandanda viwanjani.

Hata hivyo, ni wazi vijana hawaambiwi ukweli, kuwa buku au 1,000 haiwapi milioni 50, wanadanganywa kuwa kwa shilingi au hela chache wanamaliza umaskini. Ni wakati sasa waambiwe kuwa kubeti kunasababisha wengi kupoteza fedha zao kila siku. Kama watabeti 1,000,000 kwa Shilingi alfu kila mtu, itapatikana bilioni (1,000,000,000) hapo itachukuliwa milioni 100 wakapewa washindi wachache.

Na nyingine milioni 900 zikabakia mikononi mwa kampuni wachezeshaji au za kubeti, hivyo vijana wengi wanapoteza mamilioni yao. Pesa kidogo haiwezi kuwapa mabilioni kama wanavyoambiwa.

Fedha nyingi kuanzia kucheza dubwi, kubeti mitandaoni, kwenye simu na kwenye ofisi zinapotea kila siku.

Tamaa ya kupata fedha nyingi kwa kutumia fedha kidogo tena bila kufanya kazi inawaangamiza vijana Afrika.

Inawezekana kwa mtindo huo, wezi wakawa wanaongezeka kila leo wakiiba mali na vitu mitaani, mijini na katika maji yanajaa wahalifu na waporaji.

Kadhalika, inawezekana maduka na biashara mbalimbali zinafilisika kwa sababu fedha zinaporwa kuelekezwa kwenye kubeti.

Afrika inazidi kuwa bara la dhiki, vijana wake wakizamishwa baharini hasa Mediterranean kila wakati wakikimbia nchi zao kwenda Ulaya na Amerika kutafuta maisha bora kisa kuna hali mbaya kwenye mataifa yao.

Wengi hawafanyi kazi badala yake wanataka mafanikio na utajiri kupitia kubeti na kujipatia fedha nyingi kwa njia rahisi bila kutoka jasho.

Itakumbukwa kuwa katika vyuo vikuu, posho za kujikimu za mabweni na za kugharamia masomo zinazotolewa na bodi za mikopo ya elimu ya huu za mataifa mbalimbali hutumiwa kubeti, kadhalika pensheni na hata mikopo inawekezwa kwenye kubashiri.

Ukweli ni kwamba, mamilioni ya Waafrika hasa vijana wanageuka maskini kwa kisingizio cha kutaka kupata pesa bila kufanya kazi.

Ni vyema Afrika ijitafakari kwenye hili la kuhamasisha umma kupata pesa nyingi bila kufanya kazi. Yote hayo yakifanikishwa na kampeni za kubet.

Watu waachane na mtindo huo unaochochea uvivu na kupotosha dhana nzima kwamba kazi ndiyo msingi wa maendeleo na sio kuwekeza kwenye kamari.

Vijana ambao hawana kazi hujiingiza kwenye vituo vya kamari kujaribu bahati zao, wapo wanaotumia simu wote wakilenga kupata pesa za chap chap kwa kubashiri.

Yote hayo yanachochewa na ahadi za kupata mamilioni kwa kutumia pesa ndogo au 'buku' tu ambacho ndicho kivutio kikubwa zaidi kwa wachezaji hao ambao kila mara wanatoka patupu licha ya kwamba wamekuwa waraibu wa kamari.

Kamari ya elektroniki kwa vijana wengi inakuwa kama kazi ya kila siku, hofu ni kwamba huenda hawafahamu kuwa kubeti ni biashara na watu wazito duniani wamewekeza hela zao.

Wanachotafuta ni wachezaji wapoteze fedha ili wafanyabiashara hao wazipate ambayo ndiyo faida wanayoitaka na ni ukweli kuwa kupoteza pesa ni jambo la kawaida kuliko kuzipata kwa wachezaji hao.

Hivi vijana hawa wasio na kazi kwanini wahatarishe fedha zao chache walizo nazo?

**MUDA UNAOPOTEA**

Ni wazi kuwa mara nyingi Afrika haiwezi kufanya kampeni bila kuwa na msaada kutoka kwa washirika wa nchi zilizoendelea wakiitwa wadau wa maendeleo.

Kampeni hizo zinaweza kuwa kutokomeza magonjwa au kuelimisha umma kuhusu tatizo ndani ya jamii. Na pengine muda wa matangazo ya kuelimisha umma ni kidogo, lakini cha kushangaza muda au (air time) inayotumiwa kutangaza kubeti ni mwingi mno.

Vyombo vya habari hasa redio na televisheni ndani ya saa 24 zinaweza kutumia pengine saa 10 nzima kutangaza matangazo ya kubeti na kuelekeza watu jinsi ya kubeti.

Kwa hakika 'air time' au muda unaotumiwa kutangaza matangazo ya kubet ni mwingi, lakini kama ungetumiwa kuhamasisha vijana kufanya kazi, kuwa wabunifu, kufikia masoko ya bidhaa zao, kujilinda na magonjwa, kuacha ulevi wa dawa haramu za kulevya, pombe na ulevi kupindukia huenda kungekuwa na mabadiliko ya tabia.

Karibu nchi zote za Afrika karibu zina bodi za kudhibiti na kutoa leseni ya michezo ya bahati nasibu ni hilo limeshika kasi.

Michezo ya kamari inayoendelea Afrika miongoni mwa mashabiki wa soka na vijana ni uwekezaji wenye thamani ya matrilioni ya dola kwa kampuni zinazoendesha lakini kwa wanaocheza hali si ya kujivunia.

**AFRIKA ISHTUKE**

Bara hili lijue ukweli kuwa wakati wanawaachia vijana wake kupoteza hata dola moja walionayo kwenye kamari au kubeti, vijana wengine duniani kama nchini China wanatengeneza bodaboda ambazo zinauzwa kila mahali Afrika.

Vijana wa Kusini ya Sahara ndiyo wanaouza vitu visivyo na thamani kama mitumba ya viatu, nguo, vyombo vya nyumbani, runinga na hata redio.

Afrika nguvu kazi yake inapotea kwa kuwaacha vijana kuendelea na kazi zisizo na tija kama kuuza doli, protekta za simu na 'foni' za masikioni.

Pikipiki za China zinatumiwa na kila mtu Afrika na vifaa vyote vinavyouzwa na wamachinga vijana kwa wazee wa Afrika vinatoka huko huko. Wanalofanya ni kukaa juu ya bodaboda na kuzitumia kila mahali hata wakikimbia kwenye kukimbiza kubeti, hilo liibue tafakari.

Hivi bara hili linajua linachofanya kwa kuwaacha vijana wake waendelee kucheza kamari Januari hadi Desemba? Ni wakati wa kujirekebisha na ikibidi kuzipiga marufuku kwa sababu kuna faida kidogo kuliko hasara kubwa iliyo mbele yake.

## TRUMP NA USHINDI MAREKANI

# Mwanamama awa kiongozi mkuu ikulu

• Bilionea namba 1 duniani kuwa waziri

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, anatarajiwa kula kiapo Januari 20, 2025, kuchukua mamlaka rasmi kwa kipindi cha miaka minne hadi 2029.

Mwanachama huyo wa Republican anaweka rekodi ya kwanza kwa kupata ushindi wa kihistoria na kurejeshwa tena katika ikulu ya White House baada ya kuongoza kwa miaka minne kisha kuangushwa na Joseph Biden lakini baadaye anarudi tena.

Trump mwenye miaka 78, anaweka historia kwa kuwa rais wa kwanza wa zamani kurejea madarakani ikiwa zaidi ya miaka 130 imepita.

Mpinzani wake, mgombea wa Chama cha Democratic, mwanamama Kamala Harris, ilidhaniwa kuwa angetoa ushindani mkali lakini matokeo ya uchaguzi yameonyesha kuwa Trump amepata kura za kutosha za ushindi wa kishindo.

Siku mbili baada ya kujitangaza kuwa mshindi, Trump, anaanza kuandaa safu yake akigusa kwanza ikulu hadi baraza la mawaziri, atakalofanya nalo kazi.

Anaanza kwa kumteua aliyekuwa Meneja wa Kampeni, Susan Summerall Wiles, ambaye sasa ni Mtendaji Mkuu wa Ikulu ya White House.

Maelezo ya Trump, kwa mwanamama huyo mwenye umri wa miaka 67 ni kutokana na kumsaidia kufikia ushindi mkubwa zaidi alioupata kisiasa katika historia ya nchi hiyo kongwe ambayo mwaka huu imeadhimisha miaka 248 tangu kupata uhuru.

Susan ndiye mkuu wa utumishi wa ikulu, akiwa mwanamke wa kwanza kushikilia wadhifa huo na mteule wa kwanza wa Chama cha Republican katika utawala huo mpya unaoingia madarakani, Januari mwakani.

Kimsingi, Susan ni Meneja wa Ikulu ya White House na ana jukumu la kuwaajiri wafanyakazi wa rais, pia wanaoshika wadhifa huo, huwaongoza kupitia Ofisi ya Rais na husimamia shughuli zote za kila siku za wafanyakazi.

Kadhalika, anahusika na kumshauri rais kuhusu masuala ya sera, kuongoza na kusimamia maendeleo ya sera hizo.

Kwa mujibu wa kambi ya Trump, Susan atakuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo.

Susie anaelezwa kuwa ni mshirika wa kisiasa anayeogopwa zaidi na anayejulikana sana Marekani na vyombo vya habari vya nchini humo.

Trump anasema katika taarifa yake kwamba, mwanamama huyo alimsaidia kufikia ushindi mkubwa zaidi alioupata wa kisiasa katika historia ya nchi hiyo.

Katika hotuba yake ya ushindi wiki iliyopita, Trump alimtaja Susan kuwa ni shujaa aliyesimama nyuma yake jukwaani. "Anafanya kazi zaidi," rais mteule anasema.

"Susie ataendelea kufanya kazi bila kuchoka, ili kufanya 'Amerika iwe kubwa tena'," anaongeza katika taarifa yake wiki iliyopita, akimaanisha kauli mbiu yake ya kampeni inayorudiwa mara kwa mara.

Wasifu uliotolewa na tovuti ya Politico mapema mwaka huu, unamwelezea Susie kama mtu anayeogopwa lakini anayejulikana kidogo. Chini ya mwaka mmoja baada ya kufanya kazi katika siasa, alijiunga na kampeni ya Ronald Reagan, kabla ya uchaguzi mwaka 1980.

Aliendelea na jukumu muhimu katika kubadilisha siasa huko Florida, anakoishi. Mwaka 2010, alimfanya Rick Scott, kuwa mfanyabiashara wa wakati huo ambaye hakuwa na uzoefu mdogo wa kisiasa, kuwa gavana wa Florida katika miezi saba tu. Scott sasa ni Seneta.

Susan alikutana na Trump wakati wa mchujo wa urais wa Chama cha Republican mwaka 2015 na kuwa mwenyekiti mwenza wa kampeni yake ya Florida. Aliendelea kushinda jimbo hilo dhidi ya Hillary Clinton, mwaka 2016.

Gavana wa Florida, Ron DeSantis, ambaye alimweka kusimamia mbio zake za ugavana zilizofaulu miaka miwili baadaye, alimwelezea Susan "bora zaidi katika biashara".



Susan Wiles, Mtendaji Mkuu wa White House. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Oktoba mwaka huu, bilionea Musk alitoa takribani dola milioni 119 kwa kamati ya hatua ya kisiasa aliyoiunda, ili kumuunga mkono Trump, kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi ya Shirikisho.



Rais mteule Donald Trump akizungumza na tajiri wa dunia Elon Musk.

### MAWAZIRI WAJAO

Trump amegusia muundo na taswira ya baraza la mawaziri, baada ya ushindi wake katika uchaguzi wa urais, huku akiashiria nia yake ya kuachana na sera ya utawala unaomaliza muda wake wa Rais Joseph au Joe Biden.

Miongoni mwa yaliyoibua maswali kwenye vyombo vya habari ni nia yake ya kumweka bilionea namba moja duniani Elon Musk, kwenye baraza hilo.

Pia, anamtaja Robert F. Kennedy, jamaa wa familia ya Rais wa zamani wa Marekani aliyeuawa kwa kupigwa risasi John F Kennedy, anasifiwa kupinga chanjo. Ni Kiongozi mkuu katika vuguvugu la kupinga chanjo.

Seneta Robert, ni mtoto wa aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Marekani na pia ni mpwa wa aliyewahi kuwa Rais wa Marekani John F. Kennedy na Seneta Ted Kennedy.

Oktoba mwaka huu, bilionea Musk alitoa takribani dola milioni 119 kwa kamati ya hatua ya kisiasa aliyoiunda, ili kumuunga mkono Trump, kwa mujibu wa Tume ya Uchaguzi ya Shirikisho.

Pia alionekana na Trump kwenye mikutano na kuandaa mahojiano ya kirafiki naye kwenye mtandao wa kijamii wa X, ambalo ndilo jukwaa lake la mtandao wa kijamii.

Timu ya mpito ya Trump kwa sasa inafanya kazi ya kuchagua wanachama wakuu wa utawala unaokuja wa Republican, wakiwamo wakuu wa idara zote 15 za utendaji, kama vile makatibu wa serikali na ulinzi, kuanzia Januari 20, mwakani.

### ELON MUSK

Tajiri wa dunia na mwenye ushawishi anavutwa kwenye siasa hasa utawala ujao wa Trump, inaeleza tovuti ya CNN.

Kwa mujibu wa tovuti ya Forbes ana utajiri wa dola bilioni 304 kwa takwimu za mwishoni mwaka uliopita.

Bilionea huyo wa teknolojia na masuala ya kielektroniki, amekuwa akionekana katika hoteli ya Palm Beach, Florida, karibu kila siku, tangu Trump aliposhinda uchaguzi wiki iliyopita, akila naye kwenye ukumbi jioni na kujumuika na familia yake kwenye uwanja wa gofu.

Musk amekuwa kwenye chumba hotelini hapo wakati viongozi wengi wa dunia wakimpigia simu Trump kumpongeza .

Vyanzo vimemwelezea Trump kuwa alivutiwa na Musk akisema: "Lazima tuwalinde wajanja wetu, hatuna wengi hivyo."

Anatoa maelezo hayo wakati wa hotuba yake ya ushindi, wiki iliyopita. **MITANDAO**

# AKO, TEA kuboresha miradi ya elimu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SHIRIKA la AKO Tanzania Community Support limejipanga kushirikiana na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kuboresha utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya elimu nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa AKO, Hilda Kimath, alieleza dhamira hiyo mwishoni mwa wiki alipokutana na Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dk. Erasmus Kipesha, ofisini kwake jijini hapa.

Kimath alisisitiza kuna umuhimu wa kushirikiana ili kuongeza ufanisi katika miradi yao na kupunguza changamoto za gharama na ucheleweshaji.

"Naamini tukitekeleza hii miradi kwa pamoja, tutakuwa na uhakika wa usimamizi lakini pia kuinua ubora wa miradi tunayotekeleza kwani TEA ambayo ni mamlaka ya serikali ina uzoefu wa kufanya miradi kama hii," alisema.

Naye Dk. Kipesha alipongeza juhudi za wadau hao kuchangia maendeleo ya elimu na kuongeza kuwa TEA iko tayari kufanya kazi na wadau wote kwa lengo la kuboresha mazingira ya kujifunzia.

Alitaja faida za wadau kuchangia maendeleo kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa, ikiwamo kutambuliwa rasmi na kupewa cheti cha utambuzi, ambacho kinaweza kusaidia katika kupata nafuu ya kodi kutoka TRA.

TEA, ilianzishwa chini ya Sheria ya Mfuko wa Elimu Namba Nane ya Mwaka 2001 na ina jukumu la kusimamia Mfuko wa Elimu wa Taifa kwa ajili ya kugharamia miradi inayolenga kuboresha upatikanaji wa elimu bora na yenye usawa nchini.

# RC Dodoma awang'ata sikio wastaafu dhidi ya matapeli

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewaasa wastaafu watarajiwa wa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) kujiepusha na matapeli na kuwekeza kwenye miradi isiyo na tija.

Senyamule aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua semina ya watumishi wastaafu watarajiwa iliyoandaliwa na PSSSF.

Alisema ni muhimu wastaafu hao wakachukua tahadhari mapema kutokana na kuwapo na wimbi la matapeli wanaovizia fedha zao za mafao.

"Wakisikia kuwa umestaafu na umeshalipwa mafao yako wanajitokeza kukushauri kuhusu kuanzisha miradi lakini lengo lao ni fedha zako, hivyo jihadharini nao hao matapeli," alisema.

Aliongeza kuwa wapo matapeli wengine wamekuwa wakiwadai fedha wastaafu hao kwa madai ya kuwasaidia mafao yao kutoka haraka, hivyo watumie elimu waliyopata kuepuka mitego hiyo.

Naye Kaimu Mkurungenzi Mkuu wa PSSSF, Mbaruku Magawa, alisema mpango huo wa mafunzo kwa wastaafu watarajiwa wa mfuko huo hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuwaandaa wanachama wao wanaokaribia kustaafu.

Magawa alisema mafunzo hayo pia yanawasaidia kutumia fedha zao vyema katika uwekezaji wenye tija ili kumudu maisha mapya ya ustaafu.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mfuko huo wastaafu 3,340 wamepata semina na mafunzo hayo ya kujiandaa kustaafu ambapo wadau wengine wa kutoa huduma za kifedha na uwekezaji wamekuwa wakishirikishwa kutoa elimu.

Hata hivyo alisema mfuko huo umekuwa na utaratibu wa kutoa elimu kwa wanachama wake ya utunzaji wa fedha na kuhusu kujiandaa watakapostaafu kwenye utumishi wa umma.

Mmoja wa washiriki wa semina hiyo ambaye ni Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, alisema elimu hiyo itasaidia kuepuka matapeli wamekuwa wakiwavizia wastaafu.

Aidha, alisema watumishi wengi walizoea kupata fedha za kila mwezi hivyo wakipokea mafao ya mwisho bila kupata elimu ya uwekezaji zinawachanganya na kutumia kwenye miradi isiyo na tija.



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Watumishi wa Umma (PSSSF), Mbaruku Magawa, akitoa mada kwenye semina ya wastaafu watarajiwa ambao ni wanachama wa mfuko huo, iliyofanyika jijini Dodoma jana. .**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TARURA yamaliza kero ubovu wa barabara Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WANANCHI wa Wilaya ya Singida wameondokana na kero ya ubovu wa barabara baada ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini nchini (TARURA) Mkoa wa Singida kuendelea na ujenzi wa barabara zote zenye changamoto kwa kiwango cha lami na changarawe.

Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Singida, Gasper Deus, alisema hayo jana wakati akikagua baadhi ya barabara hizo zilizojengwa na zinazoendelea kujengwa.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida na Manispaa ya Singida kunatekelezwa miradi ya ujenzi wa barabara nane lengo ni kuhakikisha zinapitika muda wote.

Alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida kuna ujenzi wa mita 500 za barabara ya lami kwa thamani ya Sh.milioni 869 ambayo inaelekea kwenye ofisi mpya za halmashauri hiyo ambapo mita 500 za lami zilijengwa katika bajeti ya 2022/2023.

Deus alisema barabara hiyo ambayo inaanzia katika mji wa Ilongero kuelekea kwenye ofisi za halmashauri ina urefu wa kilometa 2.2 ambapo mpango uliopo ni kukamilisha barabara yote katika mwaka wa fedha wa 2026/2027.

"Barabara hii itakapokamilika itawawezesha wananchi kufika kwa haraka kwenda kupata huduma katika ofisi za halmashauri na matibabu katika kituo cha afya na wanafunzi wanaosoma Shule ya Msingi Ilongero kuwahi masomo," alisema.

Aliongeza: "Barabara nyingine inayotekelezwa ujenzi kwa kiwango cha changarawe ni ya Itaja -Mumbii yenye urefu kilometa 5. 4 ambayo inaviunganisha vijiji hivyo na inajengwa kwa gharama ya Sh.milioni 221.6 kutokana na fedha za mfuko wa jimbo," alisema.

Deus alisema katika Halmashauri ya Manispaa ya Singida barabara zilizojengwa ni pamoja na Barabara ya Mnung'una -Kwa Askofu yenye urefu wa mita 460 ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami kwa Sh.milioni 476 kwa fedha za mfuko wa barabara.

Alisema ujenzi wa awamu ya pili ambayo itahusisha kilometa 1.3 kwa kiwango cha lami itajengwa kwa ufadhiri wa Benki ya Dunia (WB) kupitia Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji Tanzania (TACTIC).

Deus aliongeza barabara nyingine iliyojengwa ni Mungumaji yenye urefu wa mita 700 ambayo imejengwa kwa kiwango cha lami kwa thamani ya Sh.milioni 659 ambayo ujenzi wake ulikamilika Agosti mwaka huu.

Alisema barabara hiyo ambayo jumla ina urefu wa kilometa 8.8 awamu ya kwanza zilijengwa mita 100 kwa ufadhili wa WB.

Aidha, aliwaomba wananchi kutoa ushirikiano kwa kulinda barabara miundombinu isiharibiwe kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara.

# Njombe yapokea mabilioni utekelezaji wa miradi

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani Njombe imesema imepokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo imesaidia wananchi kuondokana na adha ya kutembea umbali mrefu.

Hayo yalielezwa jana na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, wakati akitoa taarifa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama (NUU) ofisini kwake.

Mtaka alisema katika wilaya sita za mkoa huo zimepokea fedha kwa ajili ya miradi katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, miundombinu hali ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kutatua matatizo ya wananchi.

"Huko wilayani kuna miradi mingi sana, Jeshi la Polisi wanafursa zao na Magereza wanafursa zao lakini Zimamoto nao wanajenga lao, tunayo miradi ambayo inaendelea kutekelezwa katika ngazi ya mkoa," alisema Mtaka.

Mtaka alisema kutokana na kufanyika kwa miradi hiyo wabunge na madiwani mkoani humo hawapati shida kuelezea maendeleo yaliyofanywa na serikali.

"Kwa hiyo sisi kama mkoa tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan na nyinyi viongozi kwa namna ambavyo anatuma ushirikiano katika kutimiza majukumu haya ya serikali," alisema Mtaka.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Vita Kawawa alisema kazi ya kamati hiyo ni kukagua na kuangalia namna ya miradi inavyotekelezwa ilipofikia pamoja na uhalisia wa viwango.

"Moja ya dhumuni la ziara yetu leo tumekuja kwenye jengo la Jeshi la Polisi kuangalia hatua iliyofikia ili lianze kutoa huduma kwa wananchi," alisema.

Kawawa pia alimpongeza Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, kwa kuendesha vizuri kampeni ya udumavu ambapo alisema anayo matumaini kwamba itasaidia kupunguza tatizo hilo mkoani humo.

Ziara ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama mkoani Njombe itakagua jengo jipya la ofisi ya Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa (aliyevaa skafu), akiungana na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Tulia, kupokea msaada wa madawati 100 kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Kibenki kwa Wateja Binafsi na Mauzo kwa Wateja wa Benki ya Stanbic, Emmanuel Mahodonga (wa tatu kulia) na Meneja wa Tawi la Mbeya, Paul Mwambashi (wa pili kulia), ambapo shule hiyo itapata 50 na 50 mengine kwenda Shule ya Sekondari ya Nsalaga, mkoani Mbeya hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Wanawake bado wasiri kutoa taarifa za ukatili'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAWAKE katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mkoani Njombe bado wanakabiliwa na tatizo la kutoripoti matukio ya ukatili wa kijinsia, ikiwamo kipigo ambayo wanafanyiwa na wanaume zao kwa kuhofia ndoa kuvunjika.

Hayo yalielezwa juzi na Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, Herieth Magaji, wakati akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu.

Magaji alisema kitengo cha ustawi wa jamii kipo kwa ajili ya kusuluhisha migogoro na siyo kuvunja ndoa.

"Kinamama wanaonewa, wanapingwa na wakati mwingine wanaingiziwa chupa sehemu za siri lakini hawasemi, wanasema kwamba mimi navumilia ndoa ndugu zangu watanicheka, majirani watanishangaa lakini pia watoto watashi na nani," alisema Magaji.

Hata hivyo, Magaji alisema pindi unapotoa taarifa ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia itasaidia kuwaelimisha na kuwapatanisha ili kuweza kulea familia kuwa bora.

"Unapotoa taarifa sisi hatuna maana tunaachanisha ndoa yako au tunakwambia uondoke kwenye ndoa yako bali tunasuluhisha mgogoro wako, tunasuluhisha kupitia kanuni na sheria ili uweze kuendelea kuishi kwa amani siyo kwamba sisi tunatenganisha," alisema.

Magaji alibainisha kuwa matukio mengi ya ukatili kwa wanandoa yanakuwa yamefanyika kwa muda mrefu bila ya kuripotiwa na matokeo yake hadi yanasababisha madhara.

"Tunakesi kama hizi nyingi sana, ukija kwenye upelelezi wetu, uchunguzi wa kijamii wanajamii wanatumbia hao ni muda mrefu sana wanapigana, huyo mama ni muda mrefu anapingwa mpaka kuingiziwa chupa lakini hasemi ni msiri sana kisa anavumilia ndoa," alisema Magaji.

Magaji alisema uwepo wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia nchini zimesaidia kupunguza kesi hasa za ubakaji kwa sababu ya hatua ambazo zinachukuliwa kupitia vyombo vya dola.

Kwa upande wa mkazi wa Njombe Mjini, Farijika Gadau, alisema wanawake wengi bado wanakabiliwa na uoga na kutokujiamini pamoja na vitisho kutoka kwa wanaume pindi anapomfanyia ukatili.

"Kwa sababu mwanaume mwengine anampiga mke wake na kumsisitiza kwamba ukienda kusema sehemu yeyote nitakuua kwa hiyo ule uoga unachangia mwanamke ashindwe kusema kwa kuogopa vitisho," alisema Gadau.

Gadua aliwataka wanawake kuacha kuwa wavumilivu katika kufanyiwa matendo ya kikatili na badala yake wabadilike kuokoa maisha yao.

# Wanafunzi wasioona wapewa msaada vyakula, vifaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WANAFUNZI wenye ulemavu wa macho katika Shule ya Msingi Kibena iliyoko Halmashauri ya Mji wa Njombe, wamepatiwa msaada wa vyakula na vifaa vya shule na wadau wa elimu.

Akizungumza juzi baada ya kutoa msaada huo, mdau wa elimu Ezekiel Tweve alisema ameguswa kulisaidia kundi hilo kwa sababu ya matatizo wanayopitia na kisha kuahidi kuona namna ya kusaidia watoto wenye shida ya macho.

"Kwa wale wenye tatizo la macho tutawasaidia vitendea kazi ambavyo vitawasaidia katika maisha yao kwa namna moja au nyingine," alisema Tweve.

Naye Askofu wa Kanisa la TCCT, Victoriano Mhapa, alisema Waraka wa Yakobo Sura ya Kwanza mstari wa 27, neno linasema dini iliyo safi isiyo na taka mbele za Mungu baba ni kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao na kujilinda na dunia pasipo mawaa yoyote.

Baadhi ya wanafunzi akiwamo, Franco Mwalongo alimshukuru mdau huyo kutoka LBL kwa kuwapa wanafunzi hao vyakula na mahitaji ya shule, huku wakiomba wadau wengine kuwaunga mkono jitihada hizo.

"Tunashukuru kwa kuja kutembelea na kutupa msaada lakini tunaomba wadau wengine kuendelea kujitokeza kutusaidia kwa sababu bado tunayo matatizo mengi," alisema Mwalongo.

Kwa upande wake, Mwalimu Winfrida Mvingira alisema katika shule yao wanao watoto wenye mahitaji maalumu 74 na kushukuru kwa vifaa na mahitaji ambayo yatawasaidia kujifunza katika masomo yao.

Ofisa Ustawi wa Jamii Halmashauri ya Mji wa Njombe, Veronica Muyango, alisema popote atakapoonekana mtoto mwenye mahitaji maalumu asifichwe badala yake apelekwe shule.

"Tunashule yenye miundombinu rafiki ya wao kusoma na kuna walezi na wanapata mahitaji, hivyo siyo vizuri wazazi au walezi kuficha watoto hawa na naiomba jamii tushirikiane kuwafichua," alisema Veronica.

Aidha, Ofisa Ustawi wa Jamii huyo, pia aliwashukuru wadau mbalimbali mjini humo kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu na kisha kuhimiza jamii kutonyima haki ya kupata elimu watoto wenye uhitaji.

HABARI ZANZIBAR

# Serikali yataja faida Bonanza la Utalii Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema uzinduzi wa Bonanza la Sita la Utalii Kisiwani Pemba unalenga kuleta uwelewa na kukifungua kisiwa hicho kama kitovu cha utalii.

Alisema hayo wakati wa uzinduzi wa bonanza hilo linalotarajiwa kufanyika Novemba 27 hadi 30 mwaka huu visiwani Pemba.

Alisema bonanza hilo linaendelea kuboresha taswira ya Pemba kimataifa kama kituo cha michezo, urithi na utalii endelevu ikiwa ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Zanzibar.

Alisema utalii wa michezo una nafasi kubwa katika kuongeza hamasa, kushawishi vijana na jamii kushiriki na kuvutia watalii wa ndani na nje.

Alisema katika bonanza la mwaka huu jumla ya michezo sita itachezwa kwa kushirikisha washiriki kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar.

Alitaja michezo hiyo ni mashindano ya ngalawa, kuogelea, gwaride la punda, mchezo wa ng'ombe pamoja na kuendesha baiskeli na riadha.

Alisema bonanza hilo lengo kubwa ni kuifungua Pemba kama kitovu cha utalii na kuongeza idadi ya watalii wanaotembelea Kisiwani Pemba.

Alisema pia kukuza uchumi wa Pemba kupitia ajira na utali na kuvutia wawekezaji katika utalii wa michezo, urithi na afya na kuchochea miundombinu inayoendelea pamoja na utalii endelevu.

"Tunatoa wito kwa wadau wote wa ndani na nje kushiriki kikamilifu katika bonanza hili ni la kipekee na lenye umuhimu wake katika kuhakikisha pemba inakuwa katika hii sekta ya utalii kutokana na fursa zilizoko," alisema Soraga.

Hata hivyo aliwataka wanawake kisiwani Pemba kujitokeza kwa wingi katika kushiriki michezo mbalimbali katika bonanza hilo ili wasiachwe nyuma na fursa zilizoko.

Naye Katibu Mtendaji Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Arif Abbas, alisema wageni wanaohudhuria tamasha hilo lazima kuheshimu mazingira na utamaduni pamoja na watu wake wa Visiwa vya Zanzibar.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, Aboud Jumbe, alisema uzinduzi huo wa awali unalenga kuwajulisha wadau kuhusu matukio ya mwaka huu pamoja na kuonesha fursa zilizopo katika sekta ya utalii.

## 'Wadau wa uvuvi, utalii hifadhini matumbawe'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Uhifadhi wa Bahari Zanzibar kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Dk. Makame Omar Makame amewataka wadau wa uvuvi na utalii kuyahifadhi maeneo ya matumbawe ya bahari ili kutunza rasilimali hiyo na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Alitoa rai hiyo juzi wakati akizungumza na wadau wa uvuvi wa Unguja na Pemba katika mafunzo ya siku moja yanayohusu uhifadhi wa matumbawe kupitia mradi wa hifadhi matumbawe.

Alisema matumbawe ni rasilimali muhimu katika sekta ya uvuvi nchini kutokana na idadi kubwa ya watalii wanaofika nchini wanatembelea maeneo hayo kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za kitalii.

Alisema kuwa mbali na matumbawe kutumika kwa shughuli za kitalii pia yanatumika kwa ajili ya uvuvi kutokana na maeneo hayo kuzalisha samaki wengi na wavuvi kunufaika, hivyo ni vyema kuyahifadhi ili yaweze kuwaletea tija.

Alisema kuwa kutokana na umuhimu wa matumbawe idara kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeyahifadhi maeneo 14 kwa Unguja na Pemba yenye matumbawe mengi.

Dk. Makame akitaja sababu ya kuyahifadhi maeneo hayo ni pamoja na kuwa na matumbawe mazuri, hivyo wameona wayahifadhi ili yasiendelee kuharibiwa.

Mratibu wa mradi wa mifadhi matumbawe Tanzania, Godfrey Ngupula alisema lengo la mradi huo ni kukuza uwelewa wa hifadhi wa matumbawe kwa wadau mbalimbali nchini.

Akizungumza athari ya kutohifadhiwa kwa matumbawe alisema kwa Tanzania zaidi ya asilimia 80 ya wavuvi wote wanategemea matumbawe kwa ajili ya uvuvi, hivyo iwapo matumbawe hayatahifadhiwa yatapoteza uzalishaji wa samaki baharini.

Washiriki wa mafunzo hayo walisema watahakikisha wanachukua jitihada mbalimbali ili kulinda rasilimali ya matumbawe inatunzwa na kuimarika kwa faida yao na vizazi vijavyo.



Wafanyakazi wa Kampuni ya Ujenzi ya Sinohydro wakijenga chemba ya maji ya mvua katika ujenzi unaoendelea wa barabara ya mabasi ya mwendo kasi Posta jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Serikali kuendeleza upandaji, utunzaji miti ya asili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kufanya jitihada ya kusimamia suala la upandaji wa miti na utunzaji wa miti ya asili katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo wakati akizungumza na wadau na washauri wa kutunza miti ya asili na kupunguza hewa ukaa.

Alisema miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na wadau na taasisi kushirikiana kwa pamoja katika kuhakikisha wanapanda miti katika maeneo ambayo yameathirika.

"Ni muhimu kupanda miti mingi ya asili na miti ya kivuli hususani katika Manispaa ya Mji Mkongwe ambapo hali hiyo itasaidia kuweka mandhari nzuri na yenye haiba ya kuvutia na kupelekea kupatikana hewa safi na kupunguza hewa ukaa Zanzibar," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wananjamii kuachana na ukataji miti ovyo na badala yake kupanda miti ambayo itasaidia kupunguza mmomonyoko wa ardhi.

Aidha, Shamata alisema kuwepo kwa miti mingi Zanzibar kutapunguza hewa ukaa ambayo ni chanzo cha kupungua kwa mvua, kutaongeza upatikanaji wa dawa za asili, chakula cha wanyama na binadamu pamoja na mazalia ya wanyama na shughuli za utalii.

Naye Mhadhiri Mwandamizi Mshauri wa mradi wa kutunza miti asili na kupunguza hewa ukaa kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Dk. Abdalla Ibrahim Ali, alisema kuwa ujenzi wa barabara unaoendelea umechangia ongezeko la ukataji wa miti kiholela jambo linaloweza kuleta madhara makubwa ya uharibifu wa hali ya hewa nchini.

Aidha, alisema Zanzibar ina hazina kubwa ya miti asilia ikiwamo miti ya dawa ambapo kwa sasa baadhi ya miti hiyo imeanza kupotea na miti mengine iliyokuwepo katika maeneo ya Mji Mkongwe ya Manispaa ya Mji wa Unguja na Pemba imeendelea kubakia kuwa kivutio na alama muhimu.

Wakati huo huo, Waziri Shamata alikutana na kuzungumza na ujumbe wa wataalamu kutoka nchini Ujerumani katika Manispaa ya Jiji la Potsdam ulioambatana na Meya wa Jiji la Manispaa ya Zanzibar, Mahmoud Mussa, waliojadiliana mambo mbalimbali yanayohusiana na namna bora ya kuimarisha ushirikiano lakini pia kutunza na kuhifadhi mazingira.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**GLORY SILVESTER MKENDA** MKAZI WA ARUSHA MJINI ANATANGAZA KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TAE751241** ILITYOTOLEWA NA IDARA YA UHAMIAJI PCO, DAR-ES-SALAAM TAREHE 20 JUN 2024 KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA KARIBU CHA POLISI AU OFISI YA UHAMIAJI ARUSHA. **PHQ/ARU/ARU/41545/2024.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**NELSON WILSON MACHUMU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1822-0068** kilichotolewa na **ANAGAMAZO SEC SCHOOL** mwaka 2009. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0368-0540** kilichotolewa na **IMBORU SEC SCHOOL** mwaka 2012. Cheti cha chuo chenye Reg. No. **SM 190294** kilichotolewa na **TUMAINI UNIVERSITY MAKUMIRA** mwaka 2015. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/TAB/NZE/1538/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAMWEL JOFREY SINDANO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4552-0044** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AGNES TRUST SEC SCHOOL** mwaka 2015. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/NJO/MAK/5254/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FULGENCE MARIO KIBIKI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 344 BJA – CHASER GX 100** yenye Chassis namba **GX 1000057134.** Engine namba **IG 6508221.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/246621/2024.**

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**RAIJA TITO MWAMPEGETE,** Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari aina ya **Toyota Calina** yenye namba za usajili **T234AAV** yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA **POLISIPHQ/DOD/DOD/50581/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**CORBINIAN MARTINIAN BANZI** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **T 188 AMD,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye. **PHQ/MOR/MOR/20680/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHABANI IDDI KUSOGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 239 ADB** aina ya **CANTER** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/MBE/MBA/33958/2024.**

## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**COLLETHA FRANCISCO LUKALA** ambaye ni msimamizi wa mirathi ya marehemu **SIMON SHALALI MASHALA** anatangaza kupotelewa na nyaraka za umiliki wa kiwanja namba **546 Kitalu "DD"** kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga. Yeyote atakaeiona nyaraka hiyo atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu Taarifa ya Polisi **PHQ/SHI/SHI/11040/2024**

## TANGAZO LA KAZI UALIMU

Tunatangaza nafasi za kazi ya Ualimu mchepuo wa Kingereza kwa masomo ya Hesabu na Maarifa ya jamii Kuanzia chekechea hadi Darasa la saba, Sifa za Chekechea ni certificate au diploma na kwa darasa la Kwanza hadi la saba ni Diploma au shahada ya kwanza ya elimu.

**Mawasiliamo 0783 298 900**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FITINA MOHAMED SALUM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 427 BFX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/248481/2024.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na...77/2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ISSA JUMA MUHAMI wa MOROGORO KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KHAMISI ISSA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 2 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 6 mwezi 11 mwaka 2024

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Kutoka Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya SIHA**

**Kituo cha SANYA JUU Mkoa wa KILIMANJARO**

**Shauri la Mirathi Na. 35 /2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU TUMAINI AITAELI MAIMU WA WANDRI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTAMBUA MSIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU YALIYOLETWA NA RODRICK AITAELI MAIMU**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi katika Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 mwezi 11 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji kuteuliwa kuwa mwamuzi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuleta Mahakani kukaguliwa.
- Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia.

Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 10 mwaka 2024

..........................................

**HAKIMU**
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA MWANZO**
**SANYA JUU**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU DODOMA**

**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA. 22000 YA 2024**

**MARIAM YAKOBO ..............................MUOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**MOSHI OMARI.................................... MJIBU RUFAA**

**KWA: MOSHI OMARI**
**POPOTE PALE ALIPO.**

**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA. 22000 YA 2024 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA DODOMA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA;** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma mbele ya **MHE. E. KAKOLAKI,** JAJI wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma, saa tatu (3:00) asubuhi siku ya Jumanne tarehe 26/11/2024.

**HIVYO, U**natakiwa ufike wewe mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.

**NA ENDAPO;** Hutafika wewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.

**IMETOLEWA;** kwa mkono wangu na Mhuri wa Mahakama leo tarehe 31/10/2024.

NAIBU MSAJILI
DODOMA

---

**Magistrates Court (Approved Form for the Primary Court**
**GN.NO 943(Contd.)** **FOMU MADAI-3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**

**Kituo cha Mabogini Mkoa Kilimanjaro.**

**Shauri la Madai 02, 2021.**

**Jina la Mdai GAUDENCE MARISHANI.**

**Jina la Mdaiwa GREGORY L MPONZI(DALALI WA MAHAKAMA).**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: GREGORY L MPONZI**
**PWANI 0717 666158/0628083179**

**Kwa kuwa Madai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai )**
**SHILINGI MILIONI MBILI (2,000,000)PAMOJA NA GHARAMA ZA UFUATILIAJI WA SHAURI LA MADAI.**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 20 mwezi 12 mwaka 2024 saa 08:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 08 mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU
HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
MABOGINI MOSHI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI**
**AT KINONDONI**

**COMMERCIAL CASE NO. 5107 OF 2024**

**BANK OF AFRICA TANZANIA LTD............PLAINTIFF**

**VERSUS**

**OSCAR LUFURANO MBEKENGA............DEFENDANT**

**TO: OSCAR LUFURANO MBEKENGA**

**NOTICE DATE FOR EX-PARTE JUDGEMENT**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed for **EXPARTE JUDGMENT** on 25th day of NOVEMBER at 10:00 a.m Before **Hon. V. KASEKO – SRM**

**YOU ARE** required to appear in this Court without failing and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

Given under my Hand and the Seal of the Court this 5th day of NOVEMBER, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE
KINONDONI DISTRICT COURT
DAR ES SALAAM
V.KASEKO. SRM

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## PM aomba msamaha kwa unyanyasaji

**WELLINGTON,** New Zealand

WAZIRI Mkuu wa New Zealand, Christopher Luxon, ameomba msamaha rasmi kwa waathiriwa wa unyanyasaji katika nyumba za kutunza watu kufuatia uchunguzi wa moja ya kashfa kubwa zaidi za unyanyasaji nchini humo.

Ombi hilo la kihistoria, lililotolewa bungeni jana, linakuja baada ya ripoti kubaini kuwa watoto 200,000 na watu wazima walio katika mazingira magumu waliteswa wakiwa katika huduma za serikali na za kidini kati ya 1950 na 2019.

Wengi wao walikuwa watu kutoka jamii za Māori na Pasifiki na wale walio na ulemavu wa kiakili au wa kimwili. Ikielezwa kuwa serikali tangu wakati huo iliahidi kurekebisha mfumo wa utunzaji.

"Ninaomba msamaha huu kwa waathirika wote kwa niaba ya serikali yangu na ya awali. Ilikuwa ya kutisha, kuvunja moyo, ni makosa, na haikupaswa kutokea kamwe, kwa wengi wenu ilibadilisha mwenendo wa maisha yenu, na kwa hilo, serikali lazima iwajibike," Luxon alisema.

Uchunguzi huo, ambao Luxon aliutaja kuwa uchunguzi mkubwa na mgumu zaidi wa umma kuwahi kufanywa nchini New Zealand, ulichukua miaka sita kukamilika na ulijumuisha mahojiano na zaidi ya manusura 2,300 wa unyanyasaji katika taasisi za serikali na za kidini.

Ripoti iliyofuata ilirekodi aina mbalimbali za dhuluma ikiwa ni pamoja na ubakaji, kufunga kizazi na kazi ya kulazimishwa.

Iligundua pia kuwa taasisi za kidini mara nyingi zilikuwa na viwango vya juu vya unyanyasaji wa kijinsia kuliko taasisi za utunzaji za serikali. **BBC**

# Muswada wa kusaidiwa kufa unavyofanya kazi Uingereza

**LONDON,** Uingereza

WATU wazima ambao wanaugua mahututi wanaotarajiwa kufariki katika muda wa miezi sita wataweza kuomba usaidizi ili kujikatia uhai chini ya mapendekezo ya sheria ya Uingereza na Wales.

Hiyo ni kwa mujibu wa muswada uliochapishwa jana ukisema madaktari wawili wa kujitegemea watalazimika kuridhika kuwa mtu anastahiki na amefanya uamuzi wake kwa hiari, na kwamba maombi pia yatalazimika kuidhinishwa na Jaji wa Mahakama Kuu.

Mbunge wa Chama cha Labour, Kim Leadbeater, ambaye amewasilisha muswada huo, alisema unajumuisha ulinzi mkali zaidi popote duniani.

Hata hivyo, wapinzani wa kusaidiwa kufa wameibua wasiwasi kwamba watu wanaweza kuhisi kulazimishwa kukatisha maisha yao, huku ikielezwa kuwa sheria za sasa nchini Uingereza zinazuia watu kuomba msaada wa kimatibabu ili kufa.

Muswada huo utahitaji wale wanaoomba kusaidiwa kufa, awe na umri wa zaidi ya miaka 18, mkazi wa Uingereza na Wales na amesajiliwa na daktari kwa takriban miezi 12.

Pia awe na uwezo wa kiakili wa kufanya uamuzi kuhusu kukatisha maisha, kueleza matakwa ya wazi, yaliyotulia na yenye habari isiyo na shuruti au shinikizo, katika kila hatua ya mchakato.

"Lazima kuwe na pengo la siku saba kati ya tathmini za madaktari wawili na siku 14 zaidi baada ya uamuzi wa jaji kabla ya mtu kusaidiwa kufa, isipokuwa wakati kifo cha mtu kinatarajiwa mara moja.

"Mtu huyo ataruhusiwa kubadilisha mawazo yake wakati wowote na hakuna daktari ambaye atalazimika kushiriki katika mchakato huo," ulisema muswada huo.

Ilielezwa kuwa sheria bado inakataza madaktari au watu wengine kukatisha maisha ya mtu. Iwapo vigezo na ulinzi vyote vinatimizwa, nyenzo ya kukatisha maisha ya mtu lazima vijidhibiti vyenyewe.

Pia ilielezwa kuwa chini ya muswada huo daktari anaweza tu kuandaa dawa/tembe au kumsaidia mtu kumeza. **BBC**



Waokoaji wakibeba miili baada ya shambulio la Israel huko Lebanon, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yaendeleza mashambulizi Gaza, Lebanon

**JERUSALEN,** Israel

MAOFISA wa Afya wa Ukanda wa Gaza na nchini Lebanon wamesema mashambulizi ya Israel yameendelea kwenye maeneo kadhaa na kusababisha vifo 11 wakiwamo watoto wawili, majeruhi pamoja na kuharibu miundombinu muhimu ikiwamo makazi.

Maofisa hao walisema shambulio la jana lililenga mgahawa ambao unatumiwa na watu waliokimbia mapigano katika eneo la Muwasi ambalo ni kitovu cha kile kilichotangazwa kuwa ni ukanda salama, na kwamba majeruhi walipelekwa katika Hospitali ya Nasser kwa ajili ya matibabu.

Ilielezwa kuwa baadhi ya picha katika eneo hilo la mkasa zilionyesha wanaume wawili wakiwavuta majeruhi waliolowa damu kutoka kwenye mabaki ya samani za mgahawa yaliokwama kwenye vifusi baada ya shambulio la bomu la kutegwa.

Shambulio hilo lilitokea saa chache baada ya Jeshi la Israel kutangaza upanuzi wa operesheni zake katika eneo hilo na kuwataka Wapalestina wanaokaa katika maeneo hayo kuondoka mara moja.

Ilielezwa kuwa maelfu ya Wapalestina wanatumia eneo la Muwasi kujihifadhi katika kambi za mahema wakikimbia mapigano katika maeneo mengine ya Gaza, eneo ambalo lilitumika kwa ajili ya kilimo kwenye pwani ya Mediterania kusini mwa Gaza.

Eneo lingine lililoshambuliwa ni kambi ya wakimbizi ya Nuseirat iliopo katikati mwa Gaza, ikielezwa kuwa iliamshwa kwa mashambulizi ya Israel na kusababisha vifo vya watu watatu akiwamo mwanamke mmoja na kuwajeruhi wengine 11, kwa mujibu wa Hospitali ya al-Awda, ambayo ilipokea majeruhi.

Mashirika ya kibinadamu na kimataifa bado yameendelea kuutolea mwito ulimwengu juu ya hali mbaya ya kiutu katika eneo la Gaza, hasa kutoheshimiwa kwa kile kilichotangazwa njia salama za kiutu.

Wakati utawala wa Rais wa Marekani Joe Biden ukielekea ukingoni Israel inakabiliwa na muda wa mwisho kuruhusu misaada ya kiutu kuingia Gaza tofauti na hapo inaweza kujihatarishia vikwazo vinavyowezekana kwa ufadhili wa kijeshi wa Marekani.

Wakati huo huo, nchini Lebanon nako mashambulizi ya anga ya Jeshi la Israel yameua takriban watu wanane na kujeruhi 14 pamoja na kusababisha uharibifu mkubwa wa majengo ya makazi.

Ilielezwa kuwa kikosi cha msalaba mwekundu nchini humo kiliendesha operesheni ya kuokoa miili kutoka kwenye vifusi vya majengo.

Mashambulizi hayo ya anga ya Israel yalikilenga kijiji cha Ain Yaaqoub katika eneo la kaskazini la Akkar, ambako ni nyumbani mwa waumini wa Orthodox na waislamu wa madhehebu ya Sunni lakini ni mbali na kitovu cha wanamgambo wa Hezbollah wenye ushawishi kusini na mashariki mwa Lebanon.

Mustafa Yacoub, mkaazi katika eneo hilo alisema hakukuwa na tahadhari juu ya mashambulizi hayo na hali ni mbaya na hofu imetawala miongoni mwa wakaazi katika eneo hilo lililoonekana kama tulivu dhidi ya mashambulizi ya Israel.

"Hii ni mara ya kwanza kwa kijiji cha Akkar kushambuliwa, hakukuwa na maonyo yoyote. Hakukuwa na tangazo lolote la kuhama kwenye jengo. Watu 30 katika jengo wameangukiwa. Wapo waliokufa na kujeruhiwa," alisema. **DW**

# SIMBA QUEENS, YANGA PRINCESS MECHI YA KISASI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba Queens, Yussif Basigi, akiapa kuwa ni lazima walipize kisasi cha kufungwa katika mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii, Oktoba 2, mwaka huu, Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema ametamba kuendeleza ubabe.

**Timu hizo zinakutana leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, kwenye mchezo wa dabi, ikiwa ni raundi ya nne ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwa upande wa soka la wanawake.**

Simba Queens ilifungwa kwa mikwaju ya penalti 4-3 na Yanga Princess kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii kuashiria mwanzo wa Ligi Kuu msimu huu ambapo zilifika hatua hiyo baada ya kumaliza dakika 90 zikiwa zimefungana bao 1-1.

Basigi, raia wa Ghana, ambaye alipewa mikoba ya kuifundisha timu hiyo baada ya kuondoka kwa Juma Mgunda, amesema wanataka kushinda mechi hiyo ili kuwapa zawadi mashabiki wa Simba ambao anajua watajitokeza kwa wingi kuja kuwashangilia na kuwapoza machungu ya kufungwa katika mchezo wa Ngao ya Jamii.

"Wachezaji wetu wote wapo vizuri kwa ajili ya mchezo huu, na wanautaka mchezo huu, wameniambia wanataka kuwafurahisha mashabiki wao ambao wanajua watajaa kuwashangilia uwanjani na wanataka kuwafuta machungu ya kufungwa katika mchezo uliopita, kwangu mimi utakuwa mchezo wa kwanza kucheza nao kwa sababu ule uliopita nilikuwa jukwaani kwa kukosa vibali, niko tayari kuwa nyuma ya vijana wangu.

Naiheshimu Yanga Princess, najua utakuwa mchezo mzuri, kwangu mimi nimejipanga kushinda mchezo," alisema kocha huyo.

Kwa upande wake, Kocha wa Yanga, Edna, alikiri kuwa mchezo utakuwa mgumu, lakini akawatahadharisha Simba Queens pamoja na uzuri wote walionao lakini huu ni mchezo wa dabi.

"Najua mchezo utakuwa mgumu kwa sababu Simba Queens ni timu ngumu, ina wachezaji wazuri na pia inaongoza ligi, haijapoteza mechi yoyote, sisi hatujapata matokeo mazuri kwenye michezo yetu ya mwanzo, lakini hii ni dabi, mechi hizi zina mipango yake, sisi kama Yanga Princess tupo tayari kwa ajili ya mchezo huu, tunataka kuendeleza kipigo kama kile cha Ngao ya Jamii," alisema.

Timu hizo zinashuka dimbani huku Simba Queens ikiongoza ligi ikiwa na pointi tisa baada ya kushinda mechi zake tatu na Yanga Princess ikiwa na pointi tatu baada ya kucheza michezo mitatu ambayo yote wametoka sare.

## *Makumbi City waitishia nyau Kipanga FC*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Kuu Zanzibar, Muembe Makumbi City wamesema wamejindaa vizuri kukabiliana na maafande wa Kipanga FC na kuwataka wapinzani wao hao kujiandaa kwa kipigo.

Timu hizo zinatarajiwa kukutana Ijumaa kwenye mchezo wa mzunguko wa 11 wa ligi hiyo katika uwanja wa Mau A

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rajab Mrisho, alisema kwake yeye hana hofu na timu yoyote atakayokutana nayo licha ya kuwa mgeni kwenye Ligi Kuu.

Alisema anawajua Kipanga FC kwa kuwafuatilia katika Ligi Kuu ya Zanzibar lakini hana hofu na mchezo huo.

Alisema amekiandaa kikosi chake kuhakikisha hakipotezi malengo ya kupata alama tatu hasa katika michezo hii ya kuelekea ukingoni mwa mzunguko wa kwanza.

Alisema anashukuru kuelekea kwenye mchezo huo mpaka sasa hana majeruhi kwenye kikosi chake kitu kinachompa matumaini ya kufanya vizuri.

Vinara hao wa Ligi Kuu ya Zanzibar inayodhaminiwa na Benki ya PBZ wanapointi 22 huku Mlandege FC wakishika nafasi ya pili wakiwa na pointi 20 sawa na Mafunzo FC wanaoshika nafasi ya tatu.

MAGONGO...



Wachezaji wa mpira wa magongo Ramadham Khatib (kushoto) na Abuu Ali wakifanya mazoezi katika uwanja wa kituo cha michezo Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bunge Bonanza kuzishirikisha Simba, Yanga

**Na Joyce Lameck**

MWENYEKITI wa Bunge Bonanza ambaye ni Mbunge wa Makete, Festo Sanga, amesema bonanza la mwakani litazishirikisha timu za Simba na Yanga.

Akizungumza jana kwenye ofisi ndogo za Bunge jijini Dar es Salaam, Sanga alisema bonanza la mwakani limepangwa kufanyika Januari 25 jijini Dodoma.

"Tumeandaa bonanza hili ambalo litahusisha timu zetu mbili kubwa za Simba na Yanga ikiwa ni mwendelezo wa mabonanza yetu, kwanza likiwa na lengo la kuimarisha mahusiano kati ya bunge na taasisi zingine, lakini pia kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kuhamasisha michezo hapa nchini," alisema Sanga.

Alisema michezo mbalimbali itafanyika ikiwa pamoja na mpira wa miguu, mpira wa pete, kuvuta kamba, mpira wa wavu, riadha na mpira wa kikapu.

Alisema bonanza hilo la mwakani limedhaminiwa na Benki ya Azania.

Kwa upande wake Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, alilipongeza Bunge kwa kuanzisha bonanza hilo na kusema ni njia mojawapo ya kuziheshimisha timu za mpira wa miguu kutokana na kubeba hisia za watu wengi.

Alisema timu hizo mbili zimekubali kushiriki katika bonanza hilo, ili kudumisha umoja katika michezo baina ya timu hizo na kuwa bonanza hilo liwe na mwendelezo wa michezo mbalimbali ambayo inapendwa na kundi la watu wengi.

Aidha, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Azania, Agustino Matutu, amesema kuwa wamejiandaa kuhakikisha bonanza hilo linakuwa na tija zaidi.

Alisema benki hiyo sio tu wadhamini lakini pia watashiriki kwenye bonanza hilo.

"Tunajivunia kuwa tumekuwa wadhamini wa bonanza hili, tunaona fahari kushiriki kwa hiyo tunawakaribisha Watanzania kushiriki bonanza hili ambalo linasaidia kujenga umoja wa taifa katika michezo kwa sababu tunawaleta wote kwa pamoja," alisema Matutu.

**Michezo mbalimbali itafanyika ikiwa pamoja na mpira wa miguu, mpira wa pete, kuvuta kamba, mpira wa wavu, riadha na mpira wa kikapu.**

## ZISIKUPITE

### ARSENAL KUMTWAA KUDUS

KLABU ya Arsenal iko tayari kutumia pauni milioni 83 kumnunua kiungo wa kati wa West Ham, Mohammed Kudus 24, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ghana akitaka kujiunga na Washikabunduki hao ili kucheza mashindano ya Ulaya. ***(Fichajes)***

### SPURS KUWAGOMEA MADRID

TOTTENHAM Hotspur iko tayari kukataa nia mpya ya Real Madrid ya kumnunua beki wa Argentina, Cristian Romero, 26. ***(Football Insider)***

### KUTOLEWA KWA MKOPO

KLABU ya Manchester United inafikiria kumtoa kwa mkopo mshambuliaji wa Uholanzi, Joshua Zirkzee, 23, Januari huku klabu za Serie A zikimfuatilia. ***(Calciomercato)***

### JUVE YAONGOZA KWA DAVID

KLABU ya Juventus iko mstari wa mbele katika mbio za kuwania kumsajili mshambuliaji wa Canada, Jonathan David, 24, kutoka Lille huku Manchester United, Liverpool na Inter Milan pia zikimwania. ***(Footmercato)***

### MAIGNAN ATAKIWA MAN CITY

MANCHESTER City imeelekeza macho yake kwa mlinda mlango wa AC Milan na Ufaransa, Mike Maignan mwenye umri wa miaka 29. ***(Mail)***

### ATAKIWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund inafikiria kumnunua kiungo wa kati wa Sunderland, Jobe Bellingham, 19, Januari. ***(Alan Nixon via Newcastle Chronicle)***

### DAVIES AITAKA BARCA

BEKI wa Bayern Munich, Alphonso Davies, 24, yuko tayari kuungana tena na kocha wa zamani Hansi Flick katika klabu ya Barcelona licha ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada kutakiwa Real Madrid na Manchester United. ***(Team Talks)***

### POGBA BASI TENA JUVENTUS

KIUNGO wa kati wa Ufaransa, Paul Pogba, 31, anakaribia kufikia makubaliano ya kusitisha mkataba wake na Juventus na kusaini klabu nyingine kama mchezaji huru pindi muda wake wa kufungiwa utakapokamilika. ***(Sky Sports)***

### SANE NJIA PANDA BAYERN

WINGA wa Ujerumani, Leroy Sane, 28, ana nia ya kusaini mkataba mpya katika klabu ya Bayern Munich, lakini mchezaji huyo bado hajafikia makubaliano kuhusu mkataba mpya. ***(Florian Plettenberg)***

### TAH NA REAL MADRID

MLINZI wa zamani wa Hispania, Sergio Ramos mwenye umri wa miaka 38, hatarejea Real Madrid lakini watasajili beki wa kati Januari huku beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani mwenye umri wa 28, Jonathan Tah akiongoza. ***(Diario AS)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# REAL MADRID HAINA MPANGO NA RAMOS

**MADRID,** Hispania

**Wababe hao wa Hispania wameorodhesha majina ya mabeki wa tatu wanaofikiriwa ku...**

REAL imeripotiwa kwamba haina mpango wa kumrejesha mchezaji wa zamani wa klabu hiyo, Sergio Ramos, Santiago Bernabeu na badala yake wamepanga orodha ya wachezaji watatu watakaoweza kuchukua nafasi za beki wa kati wa dharura.

**Kocha Carlo Ancelotti alipoteza wachezaji watatu kutokana na majeraha katika kipindi cha kwanza dhidi ya Osasuna siku ya Jumamosi.**

Rodrygo na Lucas Vazquez wote walitolewa nje ya uwanja, huku beki wa kati Eder Militao naye akiumia.

Real Madrid walithibitisha baadaye kwamba beki huyo wa Brazil aliumia goti ikiwa ni mara yake ya pili ndani ya miezi 15, na hivyo kumfanya kuwa nje kwa muda uliosalia.

Beki mwenzake wa kati, David Alaba bado hajarejea kutokana na tatizo kama hilo ambalo alikabiliana nalo mwaka jana.

Madrid haikusajili mlinzi yeyote msimu wa joto, lakini ilimwachia nahodha wa klabu Nacho Fernandez, ambaye angeweza kucheza popote kwenye safu ya nyuma.

Dani Carvajal na Aurelien Tchouameni wote wamecheza nafasi ya beki wa kati miaka ya hivi karibuni lakini pia wote ni majeruhi.

Kuongezeka huku kwa safu ya ulinzi ilimfanya kiungo wa zamani Guti kupendekeza uwezekano wa kurejea kwa gwiji mwingine, Sergio Ramos. Nahodha huyo wa zamani alikaa Madrid kwa miaka 16 kabla ya kujiunga na Paris Saint- Germain mwaka 2021.

Ramos alirejea katika klabu yake ya utotoni ya Sevilla msimu uliopita kwa mkataba mfupi wa mwaka mmoja ambao ulimalizika Juni.

Licha ya kupatikana kama mchezaji huru, Real Madrid wamejitenga na uwezekano wa kumrejesha Ramos, kwa mujibu wa jarida la Hispania na Diario AS.

# VAN NISTELROOY AONDOKA RASMI MAN UNITED



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United imetangaza kuwa kocha wa muda, Ruud van Nistelrooy ameondoka katika klabu hiyo baada ya kuwasili kwa kocha mkuu wa kudumu, Rúben Amorim juzi Jumatatu.

Van Nistelrooy alisimamia michezo minne baada ya kufukuzwa kwa Erik ten Hag, akishinda tatu na sare mmoja. Timu hiyo ilifunga mabao 11 katika kipindi kifupi cha uongozi wake.

Nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Uholanzi na gwiji wa Man United ameondoka pamoja na wafanyakazi aliokuwa nao kwenye benchi la ufundi kipindi cha Ten Hag.

"Manchester United inathibitisha kwamba, Ruud van Nistelrooy ameondoka katika klabu hii.

Ruud alijiunga tena msimu wa majira ya joto na amechukua jukumu la kuinoa timu kwa mechi nne zilizopita kama kocha mkuu wa muda," ilisema taarifa ya klabu hiyo.

"Ruud daima atakuwa gwiji wa Manchester United. Tunashukuru kwa mchango wake na jinsi ambavyo ameshughulikia jukumu lake katika muda wote akiwa na klabu.

"Daima atakaribishwa sana Old Trafford. Rene Hake, Jelle ten Rouwelaar na Pieter Morel pia wameondoka na tunawatakia kila la heri."

Van Nistelrooy alikuwa kipenzi cha mashabiki akiwa mchezaji Old Trafford, akifunga mabao 150 katika mechi 219 katika kipindi cha miaka mitano.

Hapo awali alikuwa kocha mkuu katika klabu ya PSV Eindhoven ya Uholanzi, akijiuzulu kabla ya siku ya mwisho ya msimu wa 2022-23 huku kukiwa na taarifa kwamba, uongozi wa timu hiyo haukumuunga mkono.

# De Jong fiti kuichezea Uholanzi

**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Uholanzi, Ronald Koeman anatarajia Frenkie de Jong kurejea Amsterdam Jumamosi watakapoikaribisha Hungary katika Ligi ya Mataifa ya UEFA, lakini akasema mshambuliaji Memphis Depay hajawa fiti vya kutosha kuichezea nchi hiyo.

De Jong aliichezea Uholanzi mara ya mwisho miezi 14 iliyopita dhidi ya Ireland.

Jeraha la kifundo cha mguu mara kwa mara msimu uliopita lilimfanya kukosa kushiriki michuano ya Euro 2024 nchini Ujerumani.

Alirejea kucheza na klabu ya Barcelona Oktoba Mosi.

Baada ya kurejeshwa kwa timu ya kimataifa wiki iliyopita, kulikuwa na wasiwasi alipotolewa nje akiwa amejeruhiwa wikendi akiichezea Barcelona wakati wakifungwa na Real Sociedad.

Lakini Koeman anatarajia De Jong kuwepo kwa sababu jeraha lake halikuhusiana na kifundo chake cha mguu.

"Ilikuwa maumivu madogo, sio kifundo cha mguu. Atakuwepo na tunadhania kuwa anaweza kucheza Jumamosi," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Frenkie de Jong ni uhakika wa kuchaguliwa ikiwa yuko fiti. Lakini amekuwa nje kwa muda mrefu, bado hajacheza mechi kamili."

Lakini Depay, ambaye mara ya mwisho aliichezea nchi yake kwenye michuano ya Euro na hivi karibuni alijiunga na Corinthians huko Brazil, hakuwa tayari kurejea.

"Memphis hayuko fiti vya kutosha," alisema.





# Wachezaji 8 wajiondoa kikosi cha England

**LONDON,** England

BUKAYO Saka na Cole Palmer ni miongoni mwa wachezaji nane waliojiondoa kwenye kikosi cha England kutokana na majeraha kuelekea mechi ya michuano ya Ligi ya Mataifa ya UEFA mwezi huu.

Levi Colwill, Phil Foden, Jack Grealish, Trent Alexander-Arnold, Aaron Ramsdale na Declan Rice pia hawatapatikana katika mechi dhidi ya Ugiriki na Jamhuri ya Ireland.

Hiyo kumemfanya mchezaji wa Aston Villa, Morgan Rogers kuitwa kwa mara ya kwanza katika kikosi cha England.

Wachezaji wawili Tino Livramento na James Trafford pia wameongezwa kwenye kikosi pamoja na Jarrod Bowen na Jarrad Branthwaite. Saka aliumia mguu katika wakati Arsenal ikitoka sare na Chelsea dakika ya 81.

Mchezaji mwenzake na Saka, Rice alianza pale Stamford Bridge licha ya vyanzo kuiambia ESPN kwamba alikuwa amevunjika kidole cha mguu. Kiungo huyo baadaye alibadilishwa na Mikel Merino dakika ya 71.

Baada ya mechi, kocha wa Arsenal, Mikel Arteta alisema wote wawili wameumia na watatumia muda kidogo kupona.

Kulikuwa na mashaka juu ya kuhusika kwa Cole Palmer kwenye pambano la Jumapili kutokana na majeraha, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alicheza dakika zote 90.

Alexander-Arnold alitoka nje akiwa ameshikilia msuli wake wa paja katika kipindi cha kwanza cha ushindi wa Liverpool dhidi ya Aston Villa siku ya Jumamosi.

# MSUVA ATUA KAMBINI TAIFA STARS, AONGEZA MZUKA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva, amewasili nchini na kuripoti kwenye kambi ya timu ya taifa 'Taifa Stars' kujiandaa na michezo miwili ya kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), dhidi ya Ethiopia na Guinea.

Msuva aliwasili nchini juzi akitokea nchini Iraq, ambako anacheza soka la kulipwa kwenye klabu ya Al Talaba na kuongeza 'mzuka' kwa timu hiyo kuelekea kwenye michezo hiyo.

Stars itaanza kuumana na Ethiopia nchini Congo Novemba 16 kabla ya kucheza nyumbani dhidi ya Guinea Novemba 19.

**Winga huyo ni mmoja wa wachezaji waliorudishwa kwenye kikosi cha Stars baada ya kukosekana kwa muda mrefu kabla ya Kocha Mkuu, Hemed Suleiman 'Morocco', kuamua kumwita baada ya mashabiki wengi kutaka arudishwe.**

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Clifford Ndimbo, amesema baada ya Msuva kuwasili wachezaji wengine wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi, akiwamo nahodha Mbwana Samatta, walitarajiwa kuwasili jana.

"Msuva tayari amewasili na kuripoti kambini, kesho (leo) pia tunatarajia kupokea wachezaji wengine waliosalia, kwa maana hiyo kikosi chote cha wachezaji 25 walioitwa kitakuwa kimekamilika kufikia hapo kesho (leo) kwani wachezaji walioitwa wanaocheza soka la ndani wote wameshawasili," alisema Ndimbo.

Akizungumzia maandalizi alisema wanaendelea vizuri, ambapo asubuhi wanafanya mazoezi ya utimamu wa mwili na jioni wanafanya mazoezi kwenye uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam.

"Kikosi kinaendelea na mazoezi kuelekea kwenye michezo yetu miwili ya kufuzu AFCON 2025, wachezaji wanafanya mazoezi mara mbili, wanaanza na utimamu wa mwili, na jioni wanafanya mazoezi kwenye Uwanja wa KMC, mkakati ni kuishinda michezo yote miwili kwa sababu tukifanya hivyo hatutoangalia mechi ya mtu yoyote, ila tukidondosha, ndipo tutaanza kutazama wengine na kuombeana mabaya, hatutaki hilo litokea," alisema.

Stars inashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Kundi H, ambapo imejikusanyia pointi nne, DR Congo ikiongoza kwa pointi 12 na Guinea ikiwa nafasi ya pili ikiwa na pointi sita.

Timu mbili kwenye kundi zinafuzu kucheza fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

## Yanga yaigeukia Al Hilal, Gamondi bado yupo sana

INATOKA UK. 24

delea na maandalizi ya mechi yetu dhidi ya Al Hilal ya Sudan, " alisema Ngai.

Hata hivyo zipo taarifa zinasema kuwa mpango huo ulikuwapo, lakini viongozi waligawanyika huku baadhi wakihofia presha ya mashabiki baada ya tukio hilo pamoja na kuwa ni muda mfupi uliobaki kuelekea kwenye mchezo wa kimataifa dhidi ya Al Hilal.

Zipo pia taarifa zinazosema kuwa mpango huo upo pale pale, lakini utafanyika kwa wakati unaofaa lakini si sasa huku ikidaiwa kocha raia wa Algeria, Kheireddine Madoui ndiye anayeandaliwa kuchukua nafasi yake.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ally Kamwe, amesema wameanza rasmi maandalizi ya Ligi ya Mabingwa wakiwa chini ya Gamondi na kuzima maneno yote kuwa anaondoka.

"Taarifa yetu imenyooka na haina konakona, kocha yupo sana Jangwani, mengine yatabaki ni uamuzi wa viongozi, wakiona muda wake bado atabaki, wakiona inatosha basi, lakini niseme bado kocha yupo na amekiongoza kikosi kwenye maandalizi kuelekea mchezo wetu wa kimataifa dhidi ya Al Hilal Omdurman, hatuwezi kujibu taarifa zote za mitandaoni lakini ukweli umeonekana," alisema Kamwe.

## Mabao 164 yafungwa

INATOKA UK. 24

Djuma Shaaban wa Namungo, Heritier Makambo na Shedrack Asiegbu wote wa Tabora United, Salum Kihimbwa wa Fountain Gate, Hassan Dilunga wa JKT Tanzania, Nurdin Chona na Jumanne El Fadhil wa Prisons, Stephane Aziz Ki wa Yanga, Leonel Ateba wa Simba, Marouf Tchakei wa Singida Black Stars, Ismail Mgunda wa Mashujaa FC, Feisal Salum wa Azam FC, Ibrahim Elias wa KMC na Lulihosh Heritier wa Dodoma Jiji.



Wachezaji wa kundi la Misomisondo wakitumbuiza katika kongamano la wajasiriamali linalofanyika kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mtibwa Sugar yarejea kileleni Championship*

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuenguliwa kileleni kwa wiki mbili, Mtibwa Sugar imerejea juu ya msimamo wa Ligi ya Championship baada ya kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Stand United juzi kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro.

Mtibwa ilipata ushindi huo kupitia kwa Raizin Hafidh dakika ya 45 na Omari Marungu, dakika ya 90 ambayo yaliwahakikishia ushindi na kurudi kileleni kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Ushindi huo umeifanya timu hiyo kuongoza ligi hiyo ikiwa kwenye raundi ya nane, ikiwa na pointi 19 katika mechi nane ilizocheza, ikishinda michezo sita, sare moja na kupoteza mchezo mmoja.

Kipigo hicho kimeiacha Stand United kusalia kwenye nafasi ya sita, ikibakia na pointi zake 15.

Geita Gold, timu ambayo kama Mtibwa, iliteremka daraja msimu uliopita, ilipata kipigo cha mabao 2-0 kutoka kwa Mbeya Kwanza, mchezo ukipigwa Uwanja wa Nangwanda Sijaona, Mtwara.

Licha ya kipigo hicho, Geita Gold bado ipo nafasi ya pili ikiwa imejikusanyia pointi 17 katika michezo minane iliyocheza Mbeya Kwanza ikipanda hadi nafasi ya saba ya msimamo ikifikisha jumla ya pointi 14.

Ikiwa ugenini, Songea United ilipata ushindi wa mabao 2-1, dhidi ya Transit Camp kwenye Uwanja wa Jamhuri Morogoro na kuipeleka hadi nafasi ya nne ya msimamo ikiwa na pointi 15.

TMA, imepaa hadi nafasi ya tatu baada ya kuichapa Green Warriors ambao 3-1, Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha. Mabao ya TMA, yaliwekwa wavuni na Abdulaziz Shahame aliyepachika mabao mawili na moja lililowekwa wavuni na Ramadhani Kapera.

Timu hiyo nayo imefikisha pointi 15, ikicheza michezo minane, ikishinda minne, sare tatu na kupoteza moja, huku Green Warriors ikiwa ya 10 na pointi 10 kibindoni.

Michezo
Jumatano Novemba 13, 2024
Nipashe



Madrid haina mpango na Ramos UKURASA 21



Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, akiwa katika mazoezi jana Uwanja wa Gymkhana kujiandaa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Hilal. **PICHA: YANGA**

# Mabao 164 yafungwa Ligi Kuu mpaka sasa

**Na Adam Fungamwango**

## ●●● Idadi hiyo ni ndogo kulinganisha na kipindi kama hicho msimu…

JUMLA ya mabao 164, yamefungwa kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya 10 na baadhi ya mechi za raundi ya 11.

**Idadi hii ya mabao ni chache ikilinganishwa na jumla ya mabao 184, yaliyofungwa kwenye michezo ya raundi 10 tu ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita.**

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo la Nipashe, mabao hayo yamefungwa na wachezaji 98, katika michezo 83 ambayo imechezwa mpaka sasa ambapo ligi hiyo imesimama kupisha kalenda ya FIFA ambapo wachezaji wamekwenda kuunda kikosi cha timu zao za taifa kwa ajili ya kutafuta tiketi ya kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), zinazotarajiwa kucheza mwakani nchini Morocco.

Kati ya mabao hayo, 19 ni ya mikwaju ya penalti, na mawili ni ya wachezaji kujifunga wenyewe.

Wachezaji waliojifunga wenyewe ni Fred Tangalo wa KMC, aliyejifunga katika mchezo ambao timu yake ilicheza dhidi ya Azam FC, Septemba 19, mwaka huu, Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, ikipokea kipigo cha mabao 4-0 na Kelvin Kijili wa Simba akijifunga Oktoba 19, mwaka huu ilipocheza dhidi ya Yanga, na lilikuwa bao pekee kwenye mchezo huo, Simba ikifungwa bao 1-0.

Katika michezo 83 iliyochezwa mpaka sasa, takwimu zinaonyesha kuwa 62 imetoa washindi na mechi 21 ziliisha kwa sare.

Takwimu zinaonyesha kuwa katika michezo 62 ambayo imetoa washindi, mechi 38 timu zimepata ushindi zikiwa nyumbani na michezo 24 imetoa washindi kwa timu zilizocheza zikiwa ugenini.

Jumla ya penalti 25 zimetolewa hadi kufikia sasa, huku 19 zikitinga wavuni na sita zikiota mbawa.

Wachezaji Jean Charles Ahoua wa Simba na Ogochukwu Morice wa Tabora United wanaongoza kwa kufunga mabao mawili ya penalti kila mmoja.

Ahoua, alifunga penalti zake mbili, Simba ikicheza dhidi ya Dodoma Jiji na kushinda bao 1-0 kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Septemba 29 mwaka huu, na dhidi ya KMC Jumatano iliyopita, Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam akiiongoza timu yake kushinda mabao 4-0.

Ogochukwu, alifunga penalti yake timu yake ilipocheza dhidi ya Pamba Jiji na kushinda bao 1-0 na Mashujaa FC, ikishinda pia bao 1-0.

Wachezaji wengine waliofunga penalti moja moja ni

INAENDELEA UKURASA 23

## Yanga SC yaigeukia Al Hilal, Gamondi bado yupo sana

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga kimeanza rasmi mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, utakaochezwa, Oktoba 26 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kikiwa chini ya Kocha Mkuu Miguel Gamondi ambaye ilitajwa kuwa angepewa mkono wa kwaheri.

Kikosi hicho juzi kilianza mazoezi kwenye Uwanja wa Gymkhana, Dar es Salaam, chini ya kocha huyo na kuvunja tetesi kuwa 'ndoa' ya kocha huyo na Yanga imevunjika na kuendelea na maandalizi bila wasiwasi wowote.

Gamondi alionekana kwa mara ya kwanza juzi baada ya mchezo dhidi ya Tabora United, Alhamisi iliyopita uliochezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi wenyeji wakipoteza kwa mabao 3-1.

Baada ya mchezo huo, kukawa na tetesi nyingi zilizomhusu kocha huyo raia wa Argentina kuwekwa kikao na mabosi wake, kueleza ni kwa nini kikosi kimepoteza michezo miwili mfululizo na kuonekana kushuka uwezo, huku pia kukiwa na taarifa za kutoelewana na baadhi ya wachezaji.

Pamoja na taarifa hizo, habari za ndani zinasema kulikuwa na mpango wa kumtimua, ingawa zilikanushwa baadaye.

Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Klabu hiyo, Alex Ngai, aliibuka na kusema tetesi za kwamba klabu hiyo kumtimua Gamondi na kumleta kocha mwingine hazina ukweli wowote na kuwataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutokuwa na wasiwasi wowote kwani viongozi wa Yanga bado wana ushirikiano na benchi la ufundi.

"Yanazungumzwa mengi, lakini niwahakikishie wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa viongozi wote wa Yanga wapo vizuri, tuna ushirikiano na benchi la ufundi, tutakaa na kufanya tathmini na tunaen-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >